# Nipashe

Jumanne Aprili 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580927

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US






SportPesa

TZS. 1,198,475,840

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Chanzo** cha ajali iliyoua wanne chawekwa wazi

UKURASA 4



# Maelfu wakatisha masomo msingi

• **CAG** aanika sababu kuu tatu... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua moja kati ya nyumba 103 zinazojengwa na serikali katika Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni, jana mkoani Tanga kwa ajili ya wananchi walioridhia kuhama katika Hifadhi ya Ngorongoro. **Habari Uk. 3. PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MWINYI AMPONGEZA DUNI KUONYESHA MWELEKEO MZURI KUIMARISHA SUK**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali...

UKURASA WA 4

**RAIS MGENI RASMI SIKU YA UHURU VYOMBO HABARI**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye...

UKURASA WA 5

**MBUNGE ALIYEFARIKI KUAGWA KESHO BUNGENI**

MWILI wa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Irene Ndyamkama, aliyefariki...


## Samia: Uraia pacha haumo kwenye sera ya Diaspora

UKURASA 2

# TRA yatoa msamaha

UKURASA 3


**MICHEZO** **PABLO AWAPOZA MASHABIKI SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC),Dk Peter Mathuki akisaini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu ya Kenya, Mwai Kibaki makao makuu ya EAC jijini Arusha jana. **PICHA: EAC**

# Maelfu wakatisha masomo

**Na Sanula Athanas**

MDHIBITI na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini idadi kubwa ya wanafunzi wa shule za msingi kukatisha masomo yao nchini.

CAG Charles Kichere, anabainisha dosari hiyo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12, mwaka huu na kuwa wazi kwa umma.

Katika ripoti hiyo, CAG anasema amebaini idadi kubwa ya wanafunzi kukatisha masomo kabla ya kumaliza darasa la saba.

Anabainisha kuwa Kifungu cha 4.3.1 cha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kiliweka kiwango halisi cha uwiano wa uandikishaji wa elimu ya msingi kuwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2022.

CAG anafafanua kuwa uwekezaji unaoendelea wa serikali katika elimu umesababisha kuongeza uandikishaji ambao unachangiwa zaidi na kuanzishwa kwa elimu ya msingi bila ada.

"Nilichukua sampuli za mamlaka 27 za serikali za mitaa na kubaini kuwa kati ya mwaka 2018 na 2021, wanafunzi 18,670 walishindwa kuhitimu elimu ya msingi.

"Mwenendo wa kuacha shule umekuwa ukipungua katika miaka ya hivi karibuni kutokana na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu na mpango wa serikali wa elimu bila malipo," anasema.

Kwa mujibu wa CAG, hali ni mbaya zaidi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mkoani Mara ambayo kwenye kipindi tajwa, kati ya wanafunzi 13,625 walioandikishwa, 6,060 walihitimu darasa la saba huku 7,565 wakikatisha masomo yao, ikiwa ni zaidi ya nusu ya walioandikishwa.

Hali kama hiyo imeripotiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo mkoani Tabora ambako kati ya wanafunzi 8,137 walioandikishwa, 3,729 walihitimu huku 4,408 wakikatisha masomo, ikiwa ni zaidi ya nusu ya walioandikishwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara nayo imetajwa kuwa na dosari hiyo, CAG akibainisha kuwa kati ya wanafunzi 12,775 walioandikishwa katika kipindi tajwa, 8,289 walihitimu huku 4,486 wakikatisha masomo yao, ikiwa ni zaidi ya theluthi moja ya walioandikishwa.

Ripoti ya CAG inaonyesha kwamba kati ya halmashauri 27 zilizokaguliwa, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani Shinyanga ndiyo yenye kiwango kidogo zaidi cha wanafunzi wanaokatisha masomo yao.

Kati ya wanafunzi 6,835 walioandikishwa katika kipindi tajwa hapo juu, 6,814 walimaliza masomo yao na 21 walikatisha masomo, sawa na asilimia 0.3 ya waliondikishwa.

CAG anaendelea kufafanua kuwa tathmini yake ilibainisha sababu kuu za kuacha shule kwa wasichana zilihusiana na matukio ya ujauzito yaliyochangiwa na umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni, asili ya familia na masuala ya binafsi.

"Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae programu za kuifikia jamii ili kutoa ushauri kwa wazazi kuwaandikisha watoto wao katika shule zilizo karibu.

"Pili; mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanatakiwa kuwa rafiki na ya kuvutia kwa kujumuisha nyenzo stahiki za kufundishia pamoja na kutoa elimu ya taaluma na ufundi stadi," CAG anawasilisha hoja yake.

### UANDIKISHAJI S/MSINGI

CAG pia anasema amebaini upungufu wa uandikishaji wa wanafunzi wa shule za msingi, akifafanua kuwa alifanya tathmini ya hali ya mpango wa uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi za serikali kati ya mwaka 2018 na 2021 katika mamlaka 16 za serikali za mitaa na kubaini kulikuwa na tofauti ya wanafunzi 9,427.

Anasema ingawa kuna upungufu wa idadi ya wanafunzi walioandikishwa kwa mwaka, mwenendo wa uandikishaji umekuwa ukiongezeka kwa kiasi kulinganishwa na wakati mpango ulipoanza mwaka 2019.

"Zaidi ya hayo, nimebaini changamoto kuu zinazochangia kuandikisha wanafunzi pungufu ni kuwapo kwa shule binafsi katika maeneo ya mjini. Kwa upande wa vijijini, sababu ni pamoja na kuhamahama kwa familia zinazojishughulisha na ufugaji, maeneo ya kijiografia na uelewa mdogo wa umuhimu wa elimu kwa baadhi ya jamii ambapo sehemu kubwa ya wazazi wanapendelea watoto wao kulima na kuchunga mifugo kuliko kwenda shuleni.

"Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine kuwezesha uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu na kuboresha mazingira ya shule hususani vijijini," CAG anawasilisha hoja yake.

# Samia: Uraia pacha bado kwenye sera ya Diaspora

**Na Jenifer Gilla**

Serikali imesema inakamilisha mchakato wa kutunga sera ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), lakini suala la uraia pacha halitakuwamo kwa sasa.

Hayo yalisemwa na Rais Samia Suluhu , na kufafanua kuwa lakini haki ya hadhi maalum ipo kwa ajili yao, ikihusisha na haki nyingine za msingi ikiwamo haki ya kupata ardhi, mirathi na kuwa na mstari wao katika kiwanja cha ndege.

Rais Samia alisema sera hiyo itakapokuwa tayari itasambazwa katika nchi zote ili Watanzania waishio humo watoe maoni yako kuiboresha.

Aliyasema hayo juzi alipozungumza na Watanzania waishio nchini Marekani katika jiji la Washington DC.

"Kwenye diaspora, tunamalizia sera yenu na nataka mambo ya nje watoe copy (nakala),ziletwe Marekani na kila nchi kwenye diaspora, mpitie na mtuambie kwenye ile chapter yenu mnataka kisomeke kipi. Si kila kitu mnachokitaka kitaingia humo, lakini tunataka maoni yenu," alisema Rais Samia .

Pia Rais alisema serikali inatengeneza mtandao wa kidijitali kwa ajili ya kuwasajili Watanzania waishio nje ya nchi ili kutatua tatizo la kutojulikana idadi yao ubalozini.

"Lakini nataka niwaambie kwamba hili tatizo nadhani litapatiwa solution karibuni, kwamba tunakwenda kuanzisha diaspora digital hub, ambayo ukiwa nyumbani huko hutaki kwenda ubalozini utajiandika," alisema Rais Samia.

Rais alisema mchango wa Diaspora kwa nchi ni mkubwa ikiwamo kuiletea nchi uwekezaji na fedha za kigeni ingawa hazikatwi kodi.

Aliwasihi Watanzania hao kufuata sheria za nchini humo kwa sababu kiuhalisia sio kwao hata kama watapewa uraia na ikitokea wakakamatwa kwa kutenda kosa wanahesabiwa kama ni Watanzania.

"Ukikaa vizuri wewe ni wa huku, ukifanya makosa wewe ni Mtanzania na hawatasita kukuweka kwenye ndege wakakurudisha, pamoja na uraia wako watakutrace unatoka wapi wanakurudisha, mzigo wenu huo. Kwa hiyo niwaombe sana kaeni salama, fuateni sheria za nchi. Lakini pia pamoja na kwamba una uraia wa huku usitupe nyumbani," alisema.

Rais pia alisema kuwa katika mzungumzo yake na Makamu wa Rais wa Marekani na pamoja na mambo mengine, wameona kuwa kuna haja ya kubadilisha mwelekeo wa ushirikiano wa kutoka kusaidiwa mpaka kuwekeza na kuweka sawa migongano iliyojitokeza hapo nyuma baina ya nchi hizo mbili.

"Huko nyuma tulikuwa mikono mbele, tupeni, tugawieni, lakini sasa tunakwenda kwenye ushirikiano wa wekeza tugawane faida, fanya biashara nifanye biashara , kwa hiyo tunakwenda kwenye trade and investment cooperation, hakuna tena bwana nigawie," alisema.

Alisema pia alipata nafasi ya kutembelea kampuni ya SC inayojishughulisha na kufanya utafiti kuhusu ugonjwa wa malaria na kuzungumza nao kuhusu kuvijengea uwezo vituo vya utafiti nchini ili kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.

"Sasa wanataka kuingia Tanzania kwa nguvu na tumefanya mazungumzo nao wamekubali kutusaidia kujenga capacity (uwezo) kwenye institution zetu zinazoshughulika na 'ventor control' (kuzuia maambukizi),kuna moja ipo Tanga, kuna Ifakara Reseaech Center, lakini kuna NIMRI, zote watazipa nguvu na zitakuwa center ( vituo)za kisasa," alisema Rais Samia.

Alisema mbali na mafunzo ya kuongeza uwezo kampuni hiyo imekubali kujenga vituo 200 vya afya katika mikoa ambayo bado ugonjwa huo upo juu ikiwamo Kigoma,Ruvuma,Kagera na Geita ili waweze kupata huduma za vipimo na matibabu kwa haraka.

Akiongelea hali ya maambukizi ya UVIKO-19, Rais Samia alisema kuwa kwa sasa nchi haina maambukizi hayo lakini inaendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa kila mara kunaibuka kirusi kipya.

Alisema pia nchi ipo imara kisiasa na serikali inachukua hatua za kufanya ili vyama vyote viya siasa vikae pamoja na kujadili namna ya kuendesha siasa nchini.

"Kujadili namna ya kuendesha siasa zetu nchini nimekuja na mkakati wa maneno manne: reconciliation,resilience, reforms, rebuilding of the nation.Kwa hiyo tumeanza mazungumzo na vyama vya siasa kupitia baraza lao la vyama siasa," alifafanua Rais.

Kuhusu diplomasia, Rais alisema ipo vizuri na serikali inajitahidi kuiweka Tanzania katika ramani ya ulimwengu kama ilivyokuwa enzi za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere ya kuwa moja ya nchi zinazotegemewa kidiplomasia kimataifa.

" Tunajitahidi kuirudisha Tanzania kule alipotuacha Mwl Nyerere, kwamba linapotokea jambo la ulimwengu basi katika nchi ambazo zitaulizwa maoni yao na Tanzania iulizwe maoni yake," alisema.

HABARI KITAIFA

# TRA yatoa msamaha adhabu riba ya kodi

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetoa msamaha wa adhabu na riba ya kodi kwa vyombo vya moto vilivyoingizwa nchini bila kufuata taratibu za forodha vikiwemo vile vilivyoingizwa kwa njia zisizo rasmi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi Richard Kayombo, alisema vyombo hivyo pia ni vile vilivyokusudiwa kwenda nchi jirani na vikaingizwa nchini kinyume na taratibu.

Alisema vingine ni vile vilivyoingizwa nchini kwa muda na kuzidisha muda wa kukaa nchini (Temporary importation) na vilivyotumia msamaha wa kodi kinyume cha sheria au kubadilisha umiliki bila kufuata utaratibu.

"Msamaha huu unatolewa kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 70 kifungu kidogo cha pili cha sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria ya fedha ya mwaka 2021 pamoja na kifungu cha 249 cha sheria ya usimamizi wa uhuru wa forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya 2004 ambazo zinampa kamishna wa TRA mamlaka ya kusamehe riba na adhabu," alisema Kayombo.

Aliongeza kuwa msamaha huo unatolewa kuanzia jana hadi Juni 30, mwaka huu ukiwa na lengo la kutoa unafuu kwa wamiliki wa vyombo vya moto vyenye madeni ya kodi na adhabu, ili kulipa kodi waliyokadiriwa tu bila adhabu na riba.

Pia alisema msamaha huo umelenga kujenga ushirikiano na uhusiano mwema kati ya TRA na walipakodi husika, kuwapa motisha ya kulipa kodi kwa hiari na wakati pamoja na kuweka kumbukumbu au taarifa sahihi za umiliki wa vyombo hivyo.

Aidha, alitoa wito kwa wamiliki wote wa vyombo hivyo vya moto kujitokeza ndani ya muda wa msamaha uliotolewa na kamishna mkuu ili waweze kulipa kodi halisi inayodaiwa ili kukomboa vyombo vyao.

# PM atoa maelekezo ya kuwakamilishia makazi wanaohama kutoka Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kusimamia kwa ukaribu na kuhakikisha shughuli za ujenzi katika kijiji cha Msomera Handeni mkoani Tanga zinakamilika haraka.

Ujenzi huo ni kuwezesha watu waliokubali kuhama Ngorongoro mkoani Arusha kuishi eneo hilo kwa ajili ya kupisha shughuli za uhifadhi wa wanyamapori.

Amesema Wizara hiyo inapaswa kuhakikisha inaendelea kutoa elimu kwa wakazi wa Ngorongoro walioijiandikisha kuhama kwa hiari.

"Zoezi hili linaloendelea la kuimarisha miondombinu ikiwemo upimaji wa viwanja litawanufaisha wakazi wa Msomera pamoja na wanaohamia eneo hili."

Waziri Mkuu alitoa maelekezo hayo Jumapili na kwamba miundombinu mbalimbali katika kijiji cha Msomera kilichopo Handeni ikamilike kwa ajili ya wakazi wa Ngorongoro waliokubali kuhamia kwenye kijiji hicho ili kupisha shughuli za uhifadhi kwa maendeleo ya Taifa.

Aidha, Waziri Mkuu ameitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kuandaa mazingira mazuri ya ufugaji. "Wizara hii inapaswa pia kuhakikisha kwamba kunakuwa na miundombinu wezeshi ya wafugaji yakiwamo malambo ya kunyweshea mifugo, majosho, ujenzi wa kliniki ya kutibu magonjwa ya mifugo katika eneo hilo."

Aliielekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI, iendelee kuwekeza nguvu katika kuimarisha miundombinu ya elimu. "Kama tunavyoona hapa shule ya msingi inajengwa, sekondari inajengwa, zahanati zinakarabatiwa, lakini pia ujenzi wa kituo cha afya na barabara unaendelea, ongezeni nguvu."

Majaliwa pia aliitaka Wizara ya Maji iendelee kuhakikisha kiwango cha maji katika eneo hilo kinakuwa toshelevu kwa kuchimba zaidi ili hata majosho na malambo yapate maji ya kutosha. Maji ambayo tayari yameshachimbwa na kuyapata ni mengi kuliko mahitaji lakini tuongeze kiwango."

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alisema kuwa Wizara ilipokea shilingi milioni 321 kwa ajili ya kufanya mpango wa matumizi bora ya ardhi katika kijiji cha Msomera na mpaka sasa jumla ya michoro 11 imeshakamilika ambapo michoro mitano tayari ina viwanja 14,250 na katika hivyo viwanja 5,250 tayari viko kamili.

Aliongeza kuwa wakazi hao watapewa viwanja hivyo bure. "Tunatarajia kijiji hiki kitakuwa cha mfano na hata vijiji vingine vitakuja kujifunza hapa.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema Wizara hiyo itahakikisha miradi yote ya maji katika kijiji cha Msomera inakamilika kwa wakati ili wakazi hao waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya uejnzi wa majosho mawili mapya na ukarabati wa josho moja lililopo katika kijiji hicho.







# Chanzo ajali iliyoua watu wanne

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

CHANZO cha ajali iliyoua watu wanne na kujeruhi 18 Kijiji cha Igima, wilayani Wanging'ombe, Mkoa wa Njombe kimeelezwa kuwa ni uzembe wa dereva wa gari Coaster yenye namba ya usajili T287 CCY kuigonga Coaster nyingine iliyokua mbele kwenye msafara wa magari matano.

Baada ya kugonga iliingia kwenye bonde na gari iliyogonga kwenda kugongana uso kwa uso na lori la makaa ya mawe, Barabara ya Njombe-Songea.

Kamanda wa polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 24, saa 12 jioni na magari yao yalikuwa yamebeba waumini wa umoja wa vijana wa Kanisa Katoliki (UVIKANJO) kigango cha Njombe.

"Gari hii aina ya Howo ilikua inatokea Ruvuma imebeba makaa ya mawe na gari Toyota coaster iliyokua inaendeshwa na dereva Cuthbert Kidinya ambaye alikuwa anapatiwa matibabu alifariki hospitali na dereva wa gari hili Howo lililokua linaendeshwa na Hamisi Ramadhani, mkazi wa Kimara Dar es Salaam, ameng'oka meno pamoja na kuvunjika mkono mmoja," alisema Kamanda.

"Chanzo cha ajali ni gari aina ya Toyota coaster ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki Njombe mjini kuwa kwenye msafara na magari, gari nyingine ni Toyota coaster pia yenye namba T 549 DRT ilikuwa imetangulia mbele, gari iliyogongana na lori iliigonga coaster iliyotangulia mbele," alisema.

"Matokeo yake gari ikatoka barabarani nje kabisa ya barabara eneo lile kuna kibonde, ikaingia ikaanza kutembea mule, matokeo yake gari iliyomgonga mwenzie kwa nyuma ikaanza kuyumbayumba na katika kuyumbayumba ikagongana uso kwa uso na gari ya makaa ya mawe na ndipo ajali ilipotokea," alisema Kamanda Issah.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani Njombe, Winfred Kyambile, alisema majira ya saa 1:30 usiku walipokea majeruhi 13 wa ajali ilyotokea kwenye Barabara ya Songea Makambako na mwili mmoja wa marehemu.

"Wakati tukiendelea na matibabu wengine watatu walipoteza maisha na chanzo kikubwa ni majeraha makubwa kichwani na mivunjiko kwenye sehemu za nyonga," alisema Kyambile.

Kaimu Mganga Mkuu wa hospitali ya mji Njombe, Kibena Ayoub Mtulo, alisema kwa upande wa hospitali yao walipokea majeruhi saba, wanaume watatu na wanawake wanne na miili ya watu wanne ambayo walifia eneo la ajali wote wakiwa wanawake.

Aprili 25 majira ya saa 12 asubuhi waumini wa kanisa Katholiki mjini Njombe walimininika Kanisa la Mtakatifu Joseph, Jimbo la Njombe na kueleza kuwa wamepoteza vijana mahiri walikuwa wamejitoa kwa ajili ya kumtumikia Mungu kwa hali na mali.Wakizungumzia namna ajali ilivyotokea mashuhuda, akiwamo Damian Mwalongo, alisema walikuwa wanatoka kituo cha watoto yatima Ibumila, lakini wakati wa kurudi waliona gari ambayo imebeba wenzao ikigongana uso kwa uso na gari ya makaa ya mawe.

"Ni utaratibu wa umoja wetu wa UVIKANJO kufanya matendo ya huruma kwa kutembelea wahitaji mbalimbali na siku ya JHumapili ilikuwa kituo cha yatima Ibumila, ajali hii imetupotezea wapendwa wetu ambao tuliyafanya haya kwa upendo na kujitoa," alisema Mwalongo.

Majeruhi wa ajali hiyo wamesema hawajui nini kimesababisha ajali hiyo bali wameshtukia magari yakigongana na gari ya makaa ya mawe.

Proster Mgesha alisema, "ninachokumbuka tulitoka kuwaona watoto yatima, tulikuwa tunarudi tumeingia kwenye lami tulikua kwenye msafara wa mabasi matano na gari ndogo mbili na gari yetu ilipita mabasi mengine baada ya hapo nilisikia mshtuko wala sijaona gari iliyotuvaa kwa sababu nilipoteza fahamu nimejikuta hapa hospitali," alisema.




Mtaalam wa Bidhaa za Intaneti, Tigo, Blass Abdon, akiongea na waandishi wa habari katika uzinduzi wa simu janja kutoka Vivo Mobile Tanzania, Vivo Y01, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Shadya Amiry, Mtaalam wa Mawasiliano ,Vivo Mobile Tanzania

# Mwinyi ampongeza Duni kuonyesha mwelekeo mzuri wa kuimarisha SUK

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi ameeleza kuwa ushirikiano wa pamoja unahitajika katika kuiendeleza na kuimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar wakati alipokutana na Mwenyekiti mpya wa Chama Cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, aliyekwenda kujitambulisha rasmi.

Vile vile, Rais Dk. Mwinyi alisema ujio wa kujitambulisha pamoja na kufanya mazungumzo na kiongozi huyo ni mwelekeo mzuri wa kuimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na mustakabali mpana wa kuiendeleza Zanzibar.

Rais Mwinyi alimpongeza Mwenyekiti huyo mpya wa ACT- Wazalendo Taifa kwa kuchaguliwa na chama chake kushika wadhifa huo.

Naye Duni Haji kwa upande wake alitoa shukurani kwa Rais kwa kupata fursa ya kwenda kujitambulisha pamoja na kujadili masuala mbali mbali ya mustakbali wa Zanzibar.

Alisema kuwa mbali ya mazungumzo hayo pia, amepokea wito wa Rais Mwinyi wa kutaka kukaa pamoja na kujadili masuala yenye mustakabali wa wananchi wa Zanzibar.

Alisema kuwa Rais Mwinyi mara nyingi amekuwa akisisitiza umuhimu wa kukaa pamoja na kuzungumza badala ya kubishana kwenye majukwaa na kutupiana maneno.

Kadhalika, alieleza alivyovutiwa na wito wa Rais ambao una umuhimu mkubwa juu ya mustakbali wa Zanzibar.

Alimpongeza Rais Mwinyi kutokana na ukaribisho wake na mazungumzo yao ambayo yalikuwa mazuri huku akiahidi kuwaeleza wanachama wake suala la maridhiano linavyoendelezwa kama vile ilivyokusudiwa.

"Mimi Mwenyekiti wao nimehakikishiwa na Mheshimiwa Rais kwamba hakuna tatizo ya yale yote waliyokubaliana na Marehemu Maalim Seif kwani sote tuna nia ya kuijenga nchi yetu," alisema.

Vile vile, aliwanasihi wanachama wa chama hicho kuendeleza siasa zenye tija na kuepuka vijembe majukwani kwa kuwa hatua zilizokusudiwa katika kuiendeleza Zanzibar zinakwenda vizuri.

Duni alishinda nafasi ya Mwenyekiti kwenye uchaguzi wa chama chake uliofanyika kwenye Mkutano Mkuu Maalum Januari 29, 2022.

## Rais mgeni rasmi Siku ya Uhuru wa Vyombo Habari

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya habari nchini, itakayoadhimishwa kitaifa jijini Arusha, na kilele chake Mei 3, mwaka huu.

Katika maadhimisho hayo yatakayowaleta pamoja wadau mbalimbali wa habari, taasisi za habari, yatatanguliwa na mkutano utakao kuwa na mada mbalimbali kuhusu maendeleo na changamoto za tasnia ya habari nchini

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Nevile Meena, alisema katika mkutano huo utakaofanyika kwa siku tatu kutajadiliwa mada mbalimbali ikiwemo uhuru wa habari na sheria, mazingira ya habari na vitisho vya uhuru dhidi ya habari.

Nyingine ni nafasi ya masuala ya kidijitali katika kukuza ama kutishia uhuru wa habari, huku akieleza kuwa dhima na kaulimbiu ya siku hiyo ni uandishi wa habari na changamoto za kidijiti, ambapo pia kutakuwa na utoaji wa elimu juu ya masuala ya habari katika maeneo mbalimbali.

"Hii ni fursa kwetu anapokuja Rais kwa mara ya kwanza tutapata nafasi ya kumueleza yale yanayotusibu, ili kuyapatia ufumbuzi na hii ni fursa ambayo tukiitumia vizuri inaweza kutusaidia, bado tuna kazi kubwa ya kulinda usalama wa waandishi wa habari ili kufanya kazi kwa amani, uhuru na tukiwa tunajiamini kwa manufaa ya taifa letu na watu," alisema Meena.

Aidha, alibainisha kuwa siku hiyo wanatarajia kutakuwa na washiriki zaidi ya 400 kutoka nchi tofauti, pia kutakuwa na utoaji wa tuzo kwa waliotoa mchango kwenye tasnia watakaopigiwa kura na watu mbalimbali.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Tanzania (MISA), Wakili James Marenga, alisema kuelekea maadhimisho hayo ni muhimu serikali kufanya mabadiliko ya sheria za habari ambazo zilitungwa na bunge zinazokinzana na uhuru wa vyombo vya habari.

Pia, alisema katika maadhimisho hayo watatoa mafunzo yatakayolenga kuwaongezea uelewa wadau wa habari juu ya makosa yaliyoainishwa kwenye sheria na kutolewa ufafanuzi ikiwemo kujinaisha habari za kashfa, akidai kuwa nchi nyingi zimeshaondoa kifungu hicho, huku akisisitiza ni muhimu kwa serikali nchini kukiondoa pia.

"Katika sheria hiyo mwandishi anaweza kuandika story (habari) yenye kutetea maslahi ya jamii badala yake akajikuta anaingia kwenye matatizo kwa kupewa kesi ya uchochezi hivyo nitoe wito kwa waandishi wawe makini wakati wanapotekeleza majukumu yao. Sheria zinazotungwa zisikinzane na uhuru wa habari na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeingia," alisisitiza Marenga.

Mwakilishi kutoka Vituo vya Habari vya Umoja wa Mataifa, (UNIC)-Dar es Salaam, Stella Vuzo, alisema kipindi hiki kuna mabadiliko makubwa duniani kote juu ya kuzingatia usawa wa kijinsia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ndani ya sekta ya habari.

Alisema kwa sasa katika vyombo vya habari vya kimataifa kumekuwa na idadi kubwa ya wanawake wanaohabarisha katika maeneo mbalimbali tofauti na siku za nyuma, huku akiipongeza serikali ya Tanzania kwa jitihada za kuhakikisha wanawake wanaendelezwa.

## ACT-Wazalendo yalalamikia figisu uwekaji majina mitaa

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimemwandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, kikidai uwekaji wa majina ya mitaa na barabara unaoendelea, haufuati sheria na kanuni za majina ya barabara na mitaa.

Kimesema mchakato unaoendelea unakiuka misingi ya utawala bora na kwamba majina yanayowekwa siyo yaliyopitishwa na vikao halali na kukubaliwa na wananchi.

Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Kigoma, Sendwe Ibrahim, katika taarifa yake iliyotolewa jana, alisema wameshangazwa na uamuzi wa Wakala wa Barabara Vijiji (TARURA), kuwaamulia majina ingawa sio wenye mamlaka ya Mji wa Kigoma Ujiji.

"Itakumbukwa kuwa wawakilishi wa wananchi kupitia Baraza la Madiwani la Manispaa, waliamua kutoa majina ya mitaa kwa kuzingatia historia ya mji wetu kwa kuenzi watu maarufu wa mji wetu.

"Tumeshangaa sana kuwa baadhi ya mitaa imewekwa majina ambayo hayakupitishwa katika vikao vya juu kabisa vya mkoa kama RCC, mfano ni barabara ya kutoka Soko la Mwanga kwenda Uwanja wa Ndege wa Kigoma, ambayo iliamuliwa iitwe Dk. Amani Walid Kabourou," alisema Ibrahim na kuongeza:

"Barabara ya kutoka Stesheni ya Reli kwenda Bangwe ambayo iliamuliwa kuitwa Che Guevara na Mtaa wenye Soko la Jioni ambao iliamualiwa kuitwa Mtaa wa Mzee Bakari Menge. Yote hii TARURA wamefuta kinyume na maamuzi ya vikao halali."

Ibrahim alisema, pia madiwani waliamua kuwaenzi viongozi wa dini maarufu kutoka Mkoa wa Kigoma kama vile Askofu Kahurananga, Shekhe Khalfan Kiumbe, Askofu Paul Ruzoka, Shekhe Tofiki Ibrahim Kabeke, Shekhe Iddi Kiburwa, Askofu Gerald Mpango, Shekhe Abdul Muhsin Kitumba na wengine.

# Mbunge aliyafariki kuagwa kesho bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MWILI wa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Irene Ndyamkama, aliyefariki dunia juzi katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani unatarajiwa kuagwa bungeni kesho.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alitoa, taarifa hiyo jana bungeni baada ya kutoa taarifa ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge hadi Aprili 27, mwaka huu kufuatia kifo cha mbunge huyo.

Kwenye taarifa yake, Dk. Tulia alisema mwili wa Irene utaletwa bungeni Aprili 27 kwa ajili ya kuagwa na wabunge, unatarajiwa kuzikwa Aprili 29, mkoani Katavi.

Dk. Tulia alisema: "Waheshimiwa wabunge kwa masikitiko makubwa naomba kuwatangazia kifo cha mbunge mwenzetu, Irene Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa."

Aliongeza: " Irene Ndyamkama alifariki jana (Jumapili) katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha alikokuwa akipatiwa matibabu, aliugua ghafla akiwa safarini kuelekea Dar es Salaam, akalazimika kukimbizwa hospitalini kwa matibabu ya haraka. Naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia ya marehemu, ndugu jamaa na wananchi wa Mkoa wa Rukwa".

**KUAHIRISHWA SHUGHULI ZA BUNGE**

Dk. Tulia alisema : "Kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge, tunapofiwa na mbunge mwenzetu, siku za kazi kuna kuwa hakuna kikao cha Bunge ili kupata fursa ya kuomboleza msiba huu na kujiandaa kuupokea mwili. Hivyo naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatano."

**WABUNGE ZAIDI WAMUELEZEA**

Baada ya Spika Dk. Tulia kuahirisha shughuli za Bunge, wabunge mbalimbali walimuelezea marehemu Irene namna alivyokuwa enzi za uhai wake ndani na nje ya Bunge.

Wakizungumza na Nipashe wabunge hao walisema alikuwa ni mchapakazi, mcheshi, michango yake bungeni ililenga kuwatetea vijana na kinamama hususani wa Mkoa wa Katavi.

Wamesema enzi za uhai wake Irene alikuwa akishikamana na wabunge wenzake, kwamba kwenye shughuli za kijamii alikuwa mstari wa mbele katika kutoa mchango.

Mbunge wa Mvumi (CCM), Livingstone Lusinde, alisema enzi za uhai wake Irene alikuwa ni kijana mzuri, alishirikiana na wabunge wenzake, alitoa michango mizuri bungeni.

"Alikuwa ni mbunge mcheshi, mchangamfu. Kwenye mambo serious (ya maana), alikuwa akijitokeza. Muda wote alikuwa akizungumzia masuala ya vijana. Ijumaa nilikuwa naye na tuliongea mambo kadhaa," alisema Lusinde.

Mbunge wa Chaani, Juma Usonge Hamad (CCM), alisema Irene alikuwa mjumbe mwenzake katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Alisema: "Tulikuwa na safari ya kuelekea Dar es Salaam kukagua shughuli za viwanda, tulipokuwa njiani alizidiwa. Kwenye kamati alikuwa anachangia vizuri na alikuwa ni mchapakazi. Ninaweza kusema tumepoteza mbunge hodari."

Mbunge wa Kibaha Vijijini (CCM), Michael Mwakamo, alisema kifo cha Irene ni msiba wenye majonzi kwa sababu alikuwa na mshikamano na umewagusa wabunge wote.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, alisema: "Ni jambo zito kulizungumzia. Irene ninamfahamu sana kwa sababu mimi ni Makamu Mwenyekiti wa wabunge vijana bungeni, Irene alikuwa akichangia sana masuala ya vijana.

Alisema Irene alikuwa kiungo muhimu, amefariki akiwa na miaka 35, hivyo alikuwa bado anguvu ya kulitumikia Taifa.

Mbunge wa Dodoma Mjini (CCM), Anthony Mavunde, alisema: "Nampa pole Spika na wabunge wote kwa msiba huu. Irene enzi za uhai wake alikuwa ni mcheshi sana. Aliwasimamia na kuwatetea wanawake wa Mkoa wa Katavi. Alama aliyoiacha tutaikumbuka. Ni msiba mkubwa, tunamuombea kwa Mungu."




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Aliyoibua CAG kuhusu ARV yashughulikiwe

**SEHEMU** ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imebainisha kuwapo dawa zenye thamani ya Sh. bilioni 23.04 zilizokwisha muda wake katika maghala ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Ukaguzi huo uliofanywa mwaka wa fedha 2020/21 ripoti yake ilishakabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, na Bunge kwa ajili ya kujadiliwa na wawakilishi wa wananchi, kwa mujibu wa sheria.

Alifafanua kuwa kiwango cha kwisha muda wa dawa kwa mwaka wa fedha 2020/21 kilikuwa asilimia tano ya gharama za mauzo ya Sh. bilioni 196.83 sawa na kiwango kilichoripotiwa mwaka 2019/20 cha asilimia tano.

Pia, kiwango hicho kilizidi kinachotakiwa kwa asilimia mbili kilivyoelezwa katika Aya ya 7.3.3 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za MSD wa mwezi Juni 2018, huku MSD ikiwa na jumla ya bidhaa 7,676,436 za thamani ya Sh. bilioni 22.8 zilizopitwa na muda zilizokuwa kwenye maghala ya MSD kuanzia Aprili 16, 2000 hadi Juni 30, 2021.

Pia, CAG alibainisha kuwa MSD ilipokea fedha kutoka kwa wafadhili ambazo ni Dola za Marekani 239,023.92 ili kugharamia uteketezaji dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI, na kwamba licha ya ruhusa ya kuteketeza dawa hizo kutolewa na Wizara ya Fedha na Mipango tangu Oktoba 7, mwaka 2021, hazikuharibiwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Desemba 2021.

Aliendelea kueleza kuwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alibaini kuwapo ucheleweshaji wa kuomba vibali vya uhakiki wa vifaa tiba vya kuanzia mwaka 2014 hadi Juni 2020, ambavyo ni dawa, vifaa vya matumizi ya upasuaji na vitendanishi vilivopitwa na muda kutoka katika mamlaka za serikali zinazohusika.

Ripoti ya CAG imeibua tatizo hilo, hivyo ni vyema dawa hizo zilizoachwa zikaharibika, ziteketezwe ili kuepusha madhara mengine na pengine waliokuwa wanahitaji hawakupata kwa sababu ambazo hakuna anayejua.

Pia, ni muhimu kujua vifaa vilivyostahiki kuteketezwa viliachwa kuendelea kuwapo, licha ya kuwa ni hatari kwa afya na kwa mujibu wa sheria vinapaswa kuteketezwa.

Aidha, gharama ya kuhifadhi dawa na vifaa hivyo wakati zikisubiri kuteketezwa, zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za kusaidia wananchi.

Tunatambua wapo Watanzania waliopo maeneo mbalimbali hasa ya vijijini wanatamani kupata dawa hizo, lakini huenda hawakuzipata inavyotakiwa, kwa sababu mbalimbali ambazo ni muhimu kujua ili walipakodi waweze kuelewa.

Yapo maswali mengi ya kujiuliza.

Kama nchi ina takwimu sahihi za mahitaji ya ARV maana yake inapoagiza au inapoomba msaada itaomba kwa kadiri ya mahitaji, ikiwa ni pamoja na kuweka makadirio ya watakaoongezeka kwa kuwa tayari takwimu za kuonyesha hali ya maambukizi na muda wanaotakiwa kuanza kutumia dawa hizo utajulikana.


Inapotokea dawa zinaharibika na hazijateketezwa inashangaza na kuzua maswali mengi, ndiyo maana tunaona kuna haja ya kila jambo linalozua maswali likajibiwa.

Tayari CAG amebainisha hatari iliyopo kwa wafanyakazi wa maghala yaliyohifadhi dawa hizo, jambo ambalo sio sawa.

Tunaamini penye wengi kuna mengi hasa ya watu kutaka kujitafutia fedha kwa njia haramu.

Ni muhimu ukafanyika uchunguzi kabla ya kuteketeza kujiridhisha kuwa kiwango kilichohifadhiwa ndicho kilichopo hadi siku ya uteketezaji, na kama kimepungua ni muhimu kujua zilikwenda wapi na waliofanya hivyo wachukuliwe hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge

# Elimu kuhusu Muungano ni sharti iwe endelevu



Na Sabato Kasika

**LEO** ni kilele cha maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliofanyika mwaka 1964, ambao ulizaa taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muungano unaendelea kuwa imara tofauti na nchi nyingine ambazo zilijaribu kuungana lakini zikasambaratika.

Mathalani, mwaka 1981, mataifa ya Senegal na Gambia ya Afrika Magharibi yalitia saini mkataba wa makubaliano wa kuanzisha Shirikisho la 'Sene Gambia' au SeneGambia Confederation, hata hivyo hawakufikia malengo baada ya kusambaratika.

Aidha, Ethiopia na Eretria ziliungana mwanzoni mwa miaka ya 1950 ikiwa ni juhudi za kuunganisha makoloni ya Italia , lakini hakukuwa na mafanikio na sasa ni uhasama.

Muungano kutimiza miaka 58 leo si kazi ndogo , kwani ni umri unaozidi nusu karne, angekuwa binadamu ni mtu mzima mwenye wajukuu. Katika kipindi hicho Muungano umeendelea kuwaweka Watanzania pamoja wakiendelea kuwa wamoja bila kuwapo wa Utanganyika wala fikra za Uzanzibari.

Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kujiri kwenye kilele cha maadhiimisho ya Muungano ni mashindano ya insha kuhusu Muungano kwa wanafunzi wa shule za sekondari ambayo yanatarajiwa kuibua washindi sita.

Washindi watatu watatoka Tanzania Bara na wengine watatu ni kutoka Zanzibar ambao wanatarajiwa kupewa zawadi zao leo.

Maandiko au insha hizo zinawapa fursa wanafunzi kuelezea historia ya Muungano, mafanikio na changamoto zake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, anasema Muungano unapotimiza miaka 58 ni jambo la kujivunia na kuendeleza mazuri yaliyopatikana.

Katika ufafanuzi wake, anasema kuwa lengo ni lilelile la kuelimisha umma hasa vijana, ndiyo maana wameandaa mashindano ya insha kuhusu Muungano kwa wanafunzi wa shule sita za sekondari.

Lakini, pamoja na hayo, ingekuwa ni vyema kuwapo kwa utaratibu endelevu wa mashindano ya kuandika insha kuhusu Muungano, usiosubiri maadhimisho, badala yake yafanyike kila mara.

Utaratibu huo ungepanuliwa wigo wake hadi kwa shule za msingi, wafundishwe wauelewe Muungano, kisha nao wawe wanashirikishwa kwenye mashindano endelevu ya insha kuhusu historia ya Muungano.

Ninaamini hatua hiyo inaweza kuwafanya waelewe umuhimu wa Muungano na kuwafanya wawe miongoni mwa wale wanaouenzi kwa manufaa ya pande mbili zilizoungana na kuzaliwa Tanzania.

Kwa utaratibu huo, inawezekana ikawa rahisi hata wanafunzi wanapokuwa watu wazima wakaendelea kuelezea na kuutetea kutetea Muungano mbele ya umma na kuufanya uzidi kudumu vizazi hadi vizazi.

Ukweli ni kwamba, Watanzania hawana budi kujivunia Muungano huo ambao umewafanya waendelee kuthaminiana kuheshimiana, na sasa sherehe za mwaka huu kinazinduliwa kitabu cha historia ya Muungano.

Kitabu hicho chenye lengo la kuelimisha umma kuhusu Muungano kitazinduliwa leo na Samia Suluhu Hassan, zote hizo zikiwa ni jitihada za kuelimisha umma kuuelewa kwa upana zaidi.

Hatua hiyo inaweza kuongeza uelewa zaidi kwa kuruhusu kitabu hicho kutumiwa shuleni kufundishia wanafunzi wa pande zote mbili ili wawe mabalozi wa baadaye wa Muungano huo ambao tangu mwaka 1964 haujatetereka.

Makongamono ambayo yamekuwa kwenye maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano huo ni sawa, lakini kwenye suala la mashindano ya insha lingetafutiwa utaratibu wa kuhakikisha wanafunzi kuanzia wa vijijini hadi mijini wanalielewa.

Ikumbukwe kuwa hao ndiyo viongozi wa baadaye, hivyo ni muhimu historia ya Muungano wakaielewa wakiwa wadogo badala ya kusubiri wanakuwa wakubwa na kuingia kwenye siasa ndipo wanafundishwa.

Kuwaambia vijana kuwa Muungano ni tunu, wauenzi na waulinde bila kujua historia yake inaweza ikawa vigumu kwao, hivyo ninashauri mashindano ya insha yawe endelevu na ikiwezekana historia yake ifundishwe shuleni.

## Prof. Ngowi: Biashara inahitaji mipango

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA mada za nyuma kuhusu mafunzo ya aliyekuwa mchumi mbobezi na Profesa wa Chuo Kikuu Mzumbe, marehemu Prof. Honest Ngowi, tulishaandika kuhusu mada hii ambapo aliongelea mambo ya kuzingatia unapoandika mpango wa biashara. Leo tunaangazia upande mwingine ambapo aliongelea kuhusu umuhimu wa wajasiriamali kuwa na mpango huo.

Katika somo lake la kwanza alielezea mpango wa biashara kuwa ni andiko linaloelezea kwa undani biashara inayofanywa na mhusika ambalo hutoa taswira inayoeleweka kuhusu biashara inayofanywa na mjasiriamali husika.

Aliongeza kuwa kila wazo la biashara linatakiwa kuwa na mpango wake, kwa sababu kila biashara ina malengo yake, mikakati yake na ndoto zake.Kwa hiyo kuandika mpango huo kwa biashara zaidi ya moja kutasababisha utalekelezaji wa biashara hizo kukwama.

Akiwa katika hafla iliyohusu masuala ya biashara, Prof. Ngowi alianza kusema kuwa ni muhimu kwa mjasiriamali kuwa na biashara iliyopangiliwa ili kuepuka kufanya mambo kiholela na kuishia kupata hasara au kupata faida ya kustukiza.

Alisema biashara iliyopangiliwa humsaidia msajiriamali kujua mwelekeo wa biashara yake na kitu gani anatakiwa aongeze au kupunguza. Pia humsaidia kufahamu kama anaelekea kupata faida au hasara kulingana na mwenendo anavyouona.

Alifafanua kuwa ni muhimu kwa mjasiriamali kuandaa mpango wa biashara kabla ya kuanza biashara yenyewe ili iwe mwongozo katika utekelezaji wa shughuli hiyo.

"Kwa sababu mpango wa biashara ndio utakuonyesha je, biashara nianze au nisianze?Nikianza wateja wangu wawe kina nani?Nikianza washindani wangu wawe kina nani?Nikianza mtaji naupata wapi?Kwa hiyo utakusaidia wewe mwenyewe tu kujipanga vizuri," alisema Prof. Ngowi.

Alisema kuwa mpango wa biashara ndio kitambulisho cha mjasiriamali katika masuala yanayohusisha fedha ikiwamo mikopo, ukitoa picha nzima ya biashara kama vile ina ukubwa gani na soko lake lipoje.

Vilevile alisema mpango huo hutoa maono ya mjasiriamali, hivyo hata mtu mwingine anapouona anajua ndoto, malengo na wapi mfanyabiashara huyo anataka kuelekea katika biashara zake, hivyo hata watoto wako wanaweza kuendeleza malengo yako pale anapokuwa haupo.

"Usiinuke umeacha biashara, mabilioni, matrilioni, watu wanaanza kuuana, hawajui wewe ulikuwa umefocus wapi? Ulikuwa unaenda wapi?Kwa hiyo kuna kila haja ya kuwa na mpango wa biashara," alisema.

Mchumi huyo alisema kuwa mpango wa biashara pia utamsaidia mjasiriamali kujua ni kwa namna gani atauza na kusambaza biashara yake (distribution network) kwa wateja kama vile kuuza kwa mitandao, atapeleka kwenye magulio au kusimama kwenye masoko.

Umuhimu mwingine katika mpango wa biashara kwa mujibu wa mchumi huyo, ni kumsaidia mjasiriamali katika usimamizi wa biashara yake, jambo alilolieleza kama ni changamoto kwa wajasiriamali wengi.

"Kwa hiyo ni lazima rafiki kabla hujaanza biashara kufikiria hivi ni nani atakuja kuisimamia, haya mamilioni niliyoyawekeza pale nani anafaa kuyasimamia, na sio lazima zisimamiwe na ndugu zetu, marafiki zetu na wajomba zetu wakati mwingine tujaribu kuepuka hilo," alisema.

Prof Ngowi alisema mpango huo pia hurahisisha watu kuelewa bidhaa za wajasiriamali kiundani, kwa kuwa taarifa hizo zitakuwa ndani yake, hivyo kuepuka maswali yasiyo ya lazima kutoka kwa wadau.

# 600 waunganishiwa gesi asilia majumbani Mtwara

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limewaunganisha zaidi ya wakazi 600 wa Manispaa ya Mtwara Mikindani mkoani hapa na mtandao wa matumizi ya gesi asilia majumbani.

Wakazi hao wameunganishiwa nishati hiyo kwa ajili ya kupikia tangu kuanza kwa mpango huo mapema mwaka 2020.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa shirika hilo, Adelian Kabwogi, alitoa taarifa hiyo alipokuwa akimweleza Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, Sahil Nyanzabara Geraruma, katika mkesha wa Mwenge wa Uhuru uliofanyika katika Kijiji cha Msijute Halmshauri ya Wilaya ya Mtwara kuwa wakazi hao kwa sasa wanafaidika na matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia.

Alisema hatua hiyo inawawezesha kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia na kuchangia katika uhifadi wa mazingira, na kwamba mpango uliopo ni kuwaunganisha wananchi wengi zaidi.

"Tumefanikiwa kuwaunganisha zaidi ya wakazi 600 na huduma ya matumizi ya gesi asilia majumbani katika Mji wa Mtwara hatua hii ni muhimu kwa kuwa inapunguza matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kuhifadhi mazingira" alisema na kuongeza:

"Mipango iliyopo ni kuwafikia wananchi wengi zaidi ili faida ya gesi asilia ianze kuonekana ndani ya kaya si tu kwa kutumia umeme bali kuitumia yenyewe kwa kupikia."

Alibainisha kuwa uwapo wa visima vya gesi asilia katika ardhi ya Wilaya ya Mtwara imewawezesha kutumia zaidi ya Sh. milioni 321.8/- kwa ajili ya kusaidia huduma za jamii kwa wananchi wa maeneo hayo katika kipindi cha 2014 hadi 2022.

Alitaja baadhi ya miradi iliyonufaika na fedha hizo ni uchimbaji wa visima vya maji katika kijiji cha Madimba, ujenzi wa nyumba ya mganga katika Zahanati ya Mingoji, ujenzi wa ofisi ya Mtaa wa Kiangu B, soko la kijiji cha Namindondi, visima viwili vya maji Miyuyi, ukarabati wa boti ya Polisi na ujenzi wa nyumba ya mkuu wa wilaya.

Geraruma aliipongeza TPDC na kuitaka kujikita katika utafiti wa mafuta ili Tanzania iweze kuzalisha kwa wingi na hatimaye kuchangia kushusha bei ya mafuta nchini.

"Ni muhimu zaidi kuwekeza katika utafiti wa mafuta kama Taifa ili tuwe wazalishaji wakubwa wa mafuta ili tuweze kupunguza bei ya nishati hiyo kwa wananchi wetu," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela akichukua futari katika hafla iliyoandaliwa na Benki ya KCB kwa wateja wake mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dar kujenga sekondari ya kisasa wanafunzi mchanganyiko

**Na Mary Geofrey**

MKOA wa Dar es Salaam, unatarajia kujenga shule ya kisasa ya sekondari ya wanafunzi mchanganyiko, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita itakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,000.

Shule hiyo itakuwa ya bweni na inatarajiwa kujengwa katika mwaka mpya wa fedha wa 2022/23 na itakamilika mwisho mwa mwaka huu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, aliyasema hayo jana mkoani humo, wakati akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huo, Amos Makalla, kwenye uzinduzi wa ugawaji wa vifaa vya TEHAMA kwa vituo vya walimu na shule teule katika Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa.

Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, sambamba na ugawaji wa vifaa hivyo kwa maofisa elimu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali nchini.

"Nikudokeze Waziri Bashungwa unaweza kuona shule hii ya Benjamin Mkapa ni kubwa sana kwa mkoa wetu kwa sababu inachukua wanafunzi zaidi ya 1,700, lakini tuna mpango wa kujenga shule bora ya kisasa ya mkoa itakayochukua wanafunzi wengi zaidi na ujenzi utaanza muda wowote kuanzia sasa," alisema Rugwa.

Alimueleza Bashungwa kuwa, lengo la mkoa huo ni kukamilisha ujenzi mapema iwezekanavyo ili ianze kufanya kazi kuanzia Januari mwakani.

Waziri Bashungwa alisema, vifaa vya TEHAMA vimetolewa kwenye vituo 150 vilivyopo nchini kwa ajili ya walimu kujifunza na kufundisha somo la TEHAMA.

Alitaja vifaa walivyogawa kuwa ni mashine za kutolea nakala kwenye vituo vyote, kompyuta za ofisini 600 na projekta.

Bashungwa aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini, kutenga fedha kwa ajili ya kusambaza vifaa hivyo ili lengo la serikali la kutoa elimu stahiki kufikiwa nchini.

Alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha mfumo wa kutoa elimu ya sayansi kwa njia ya televisheni nchini.

Naibu Katibu Mkuu wa TAMISEMI sekta ya elimu, Gerald Mweli, alisema serikali imeamua kufufua vituo vya kujifunzia walimu kwa kutoa mashine hizo za kisasa za TEHAMA.

Aliwataka walimu wote wanaolengwa kufikiwa na huduma hiyo ili nao watoe elimu inayoendana na viwango vya kimataifa.

HABARI KITAIFA

# Walioihujumu Ushirika Pwani waandaliwa dawa

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, amesema Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU) kinatakiwa kuwachukulia hatua za kisheria viongozi wanaotuhumiwa kukihujumu na kusababisha hasara bila kuogopana.

Kunenge amesema kazi yake kubwa atakayoifanya ni kutekeleza na kuondoa kero zilizopo upande wa Serikali hususani kwenye eneo la pembejeo na suala la kuwawajibisha wahujumu lisimamiwe na viongozi wa chama.

Mkuu huyo wa Mkoa alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CORECU uliofanyika Kibaha na kuhusisha wajumbe kutoka wilaya za Mkoa huo.

"Kuna mambo mengine mmeniomba niyachukue, ila sijayachukua ya kwenu kwakua yako ndani ya mamlaka yenu mnaweza kuyafanya, lakini hamjafanya hivyo kwa makusudi yenu bila kuona kuwa wanaoumia ni wale wananchi ambao wanawaamini nyinyi muwaongoze na waone faida ya zao la korosho."

"Yaani chama cha msingi kimemkabidhi mtu korosho tani 20 zimepotea halafu mimi ndio niende nikafuatilie na aliyekabidhiwa hayupo, kwa hili jamani haliwezekani tutafute namna ya kuwawajibisha wahusika ambao tunawajua," alisema.

Aidha, Kunenge alisema ataendelea kufanya yale anayotakiwa kufanya kama serikali ikiwamo kupata pembejeo kwa wakati

"Tumedhamiria kuleta mapinduzi katika zao la korosho kwenye mkoa wetu na ushirika mnatakiwa katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi muende sambamba na malengo yake ambayo ni kufikia uzalishaji wa tani 36 kwa mwaka 2025 na hili nina imani linawezekana kwa kasi ya uongozi huu," alisema.

Mwenyekiti wa CORECU, Mussa Hemed, alisema watatekeleza maelekezo ya Mkuu wa mkoa ikiwamo kuwachukulia hatua waliohusika na ubadhirifu kwenye ushirika.

Alisema maelekezo hayo watayafanyia kazi ndani ya mwezi mmoja ili kusafisha chama hicho na kwenda sawa na mipango waliyojiwekea ya kuleta mabadiliko.

Meneja wa CORECU mkoa wa Pwani, Mantawela Hamisi, alisema katika mkutano huo mkuu wamewaripoti kwenye vyombo vya dola viongozi wanaotuhumiwa kuwaibia wakulima hatua za kisheria zifuatwe.

Mmoja wa wajumbe wa mkutano huo, Kassim Juma ambaye ni mwenyekiti wa AMCOS ya Ikwiriri, alisema matarajio yao kwa uongozi wa sasa wa CORECU ni kuleta mabadiliko chanya kwa wakulima.

Alisema uongozi huo unatakiwa kusimamia kuondoa migogoro iliyokuwapo awali ambayo ilisababisha baadhi ya vyama kujitoa.

## Wazalishaji matofali wasisitizwa viwango

Na Joseph Mwendapole

WAZALISHAJI wa matofali wamehimizwa kuzingatia ubora na viwango katika kuzalisha bidhaa hiyo.

Mbinu hiyo imetolewa kwa wadau hao na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa kuwataka kuzalisha matofali kwa kuhakikisha wanazingatia uzalishaji wenye ubora na viwango vinavyokubalika.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi waTBS, Johanes Maganga, wakati akifungua mkutano ulioandaliwa na shirika hilo na kuwashirikisha wadau wa kuzalisha matofauli.

Alisema wazalishaji wa matofauli ni wadau muhimu katika suala la kuhakikisha wanazalisha matofali yenye ubora.

Katika majadiliano hayo wazalishaji wa matofali walitoa wito kwa TBS kuwatembelea katika maeneo yao ya uzalishaji kwa ajili ya kukagua na kuwapa mafunzo ili kuzalisha matofali yenye ubora.

Aidha, walishauri TBS kukutana na wadau wa kuzalisha matofali na kukubaliana, kuelimishana suala la 'marking' na 'grades' za matofali zitakazotumika kwa ajili ya 'marking'.

"Mfano grade A1 kwa ajili ya matofali ya inchi 4 yenye kustahimili kubeba uzito fulani kama ilivyofanyika kwa wadau wa nondo, ili kusaidia wateja kutambua aina ya tofali alilouziwa kwa urahisi na vile vile wazalishaji kuuza kulingana na ubora wa matofali," alisema John Zimbwe.

Aidha, alishauri wapatiwe elimu kuhusu mtiririko wa kuzalishaji matofali yenye bora hususani suala zima la jinsi ya kumwagilia matofali maji kwa siku. Zimbwe alishukuru TBS kwa jinsi ambavyo ilietambua umuhimu wakuwa na mkutano huo kwani wameongeza uelewa na aliahidi kufikisha elimu kwa wenzao walioshindwa kufika kutokana na kutingwa na majukumu.

Wakati huo huo, TBS imeahidi kufanyia kazi maombi na ushauri wa wazalishaji wa matofali ili kuwawezesha kuzalisha matofali yenye viwango.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)

MAADHIMISHO YA MIAKA 58 YA MUUNGANO


Dk. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Bodi ya Usimamizi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) tunaungana na Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mh. Dkt. Hussein Hassan Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na Wananchi wote katika kuadhimisha Miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.


Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

"Usalama na Afya Mahali pa Kazi huongeza tija" OSHA inasimamia hilo

Occupational Safety and Health Authority
osha_tanzania_official
TanzaniaOsha
Osha online TV

SIMU YA BURE: 0800110091/2

Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),
P.O Box 519, DAR ES SALAAM
Simu Na: +255- (0)22 -2760548/276055
Nukushi Na: (022) 27605 Barua pepe: info@osha.go.tz

## Jumuiya Wazazi CCM yajielekeza kwenye uchumi

**Na Sabato Kasika**

MJUMBE wa Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Wazazi ya CCM Taifa, Suleiman Kimei, amewataka wanachama wa jumuiya ya kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kuinuka kiuchumi, kwa kuwa siasa ni uchumi.

Kimei alitoa ushauri huo jijini Dar es Salaam juzi wakati akifungua mafunzo ya ujasiriamali kwa wanachama wa jumuiya hiyo kutoka wilaya ya Ilala na kufafanua kuwa siasa hazina budi kuendana na uchumi.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalam wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni kinachopambana na ukatili wa kijinsia, ambapo wanufaika walikuwa ni wanachama wa jumuiya hiyo toka kata 36 za Wilaya ya Ilala.

"Umefika wakati sasa kupiga hatua kwa kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ambavyo vitawasaidia kuinuka kiuchumi, kwani siasa ni uchumi, hivyo tumieni mafunzo haya vizuri ili yawanufaishe," alisema Kimei.

Aidha, aliwapongeza viongozi wa jumuiya hiyo Wilaya ya Ilala kwa kuandaa mafunzo hayo na kutaka wengine kuiga mfano huo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa wanachama wao na jumuiya kwa ujumla.

Mwenyekiti wa jumuiya hiyo Wilaya ya Ilala, Mohamed Msofe, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutaka washiriki wote kuyapeleka kwenye vikundi vyao ili kusambaza elimu ya ujasiriamali ili vijikomboe kiuchumi.

"Kumekuwapo na baadhi ya watu wanaochukua mikopo inayotolewa na manispaa bila kujipanga na kujikuta wanaitumia kwa mambo mengine, lakini kupitia mafunzo hayo tatizo linaweza kuisha," alisema Msofe.

Alisema, anaamini fedha za mikopo hazitapotelea kwenye mambo mengine na badala yake watakaokopa wataitumia kwa kile walichokusudia ili kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, Seleman Bishagazi alitaja mafunzo ambayo kituo chake kimetoa kuwa ni jinsi ya kutengeneza keki na kuipamba.

"Kutengeneza mkaa unaotokana na takataka mbalimbali, kutengeneza sabuni za kufulia, jiki, sabuni za kusugulia sinki, kutengeneza mikate bila mafuta na urembo mbalimbali kwa kutumia shanga,"alisema Bishagazi.

Bishagazi aliongeza kuwa mafunzo mengine waliyotoa kwa wanachama wa jumuiya hiyo kuwa ni ya ufugaji wa kuku na jinsi ya kuibua fursa zinazotokana na changamoto zinazomzunguka mtu.

# Wasiojulikana waiba nyaya za kopa kwenye transfoma

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

WATU wasiojulikana wameiba nyaya za kopa katika transfoma ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga na kusababisha kukosekana kwa umeme katika eneo hilo.

Vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa nyakati za usiku na watu wasiojulikana katika maeneo ya kata za Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala na Mwendakulima Manispaa ya Kahama.

Hujuma hiyo imesababisha wananchi kukosa huduma ya umeme kwa zaidi ya saa 24 tangu ulipotokea wizi huo mwishoni mwa wiki.

Hujuma hizo zilibainishwa na Ofisa Uhusiano na Huduma kwa wateja wa TANESCO wilayani Kahama, Jimmy Monyo.

Alisema vitendo hivyo ni vibaya kwa jamii, na kwamba mtu atakayebainika kuvifanya atashtakiwa kwa kosa la uhujumu kwani kufanya hivyo ni kuhujumu shirika lisiendelee kutoa huduma ipasavyo.

Alisema zaidi ya transfoma tisa zimeibiwa nyaya za kopa ambazo zinatumika kulinda transfoma isipigwe na radi wakati wa mvua na kwamba huuzwa mtaani kama vyuma chakavu.

Monyo alitaja baadhi ya maeneo ambayo transfoma zimeharibiwa kuwa ni pamoja na mtaa wa Mbulu, Mbulu Misheni, kata ya Mwendakulima, Mwendakulima shuleni, Miembeni, kijiji cha Kabale na zahanati ya Kabale.

"Tumekuwa tukishughulika kila siku kuhakikisha umeme haukatiki katiki mara kwa mara kwa wateja wetu, viwanda vyetu vinapata umeme wa uhakiki, lakini kuna baadhi ya watu wanaohujumu shirika kwa kukata nyaya kwenye transfoma, tukiwabaini watakuwa mfano kwa wengine,"alisema Monyo.

Aidha, aliwataka wananchi kutoa taarifa wakimuona mtu nyakati za usiku amepanda juu ya transfoma hata kama yuko na gari la shirika hilo na wafike wamhoji pamoja na kumuomba kitambulisho cha kazi yake na wakati mwingine wapige simu kwa namba za huduma kwa wateja ili kujiridhisha kama ni mfanyakazi wa shirika hilo.



Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana (wa tatu kushoto) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Innocent Bashungwa (kulia kwake) na baadhi ya wafanyabiashara, wakiwa katika uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 18 ya utendaji wa kampuni ya Silent Ocean yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi sekondari, vyuo vikuu kupata ufadhili 2022

**Na Julieth Mkileri,** KIBAHA

Wanafunzi 200 wa vyuo vikuu na elimu ya sekondari wamepata fursa ya ufadhili wa masomo mwaka huu.

Fursa hiyo kutoka kwa Benki ya NMB itatolewa kwa wanafunzi 150 wa kidato cha tano na sita, huku 50 kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa mwaka 2022.

Aliyetoa ahadi ya ufadhili huo ni Mkaguzi wa ndani wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, wakati wa mahafali ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Mwanalugali iliyopo Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani .

Baragomwa alisema ufadhili huo hutolewa na benki hiyo kupitia miradi yao miwili iitwayo Nuru Yangu Scholarship na Mentorship Program chini ya NMB Foundation iliyozinduliwa mwaka jana.

Aidha NMB imetoa viti 50 na meza 50 vyenye thamani ya Sh.milioni tano kwenye Shule ya Sekondari ya Mwanalugali kwa ajili ya kupunguza changamoto za shule hiyo.

"Ufadhili huu ni wa masomo kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita na kwa wale wanaoingia vyuoni kigezo kikubwa uwe umefaulu vizuri na pia wanaotoka familia duni,"alisema Baragomwa.

Alisema kuwa anaamini wahitimu wote hao wataendelea na masomo ya vyuo vikuu hivyo waachane na ile dhana potofu kuwa elimu bora inapatikana nje ya nchi kwani elimu ya Tanzania ni bora sana.

"Kwa taarifa yenu tu mimi pia ni zao la elimu hii hii na nilisoma katika shule kama hizi na nilizingatia vyema mafundisho ya walimu wangu na wazazi na mpaka leo hii nipo hapa kama mgeni rasmi nikiwa ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB,"alisema Baragomwa.

Alisema kuwa wanahamasisha wanafunzi wasome kwa bidii ili kupata viongozi bora na kuwataka walimu kufanya kazi kwa bidii ili kusaidia vijana kuinua kiwango cha elimu,kwa kuwa kufanya kazi kwa bidii kutatoa mchango mkubwa hasa katika kuitikia wito wa serikali wa kuboresha elimu.

"Wanafunzi wanapomaliza shule na kuingia mtaani, wakumbuke kuwa kuna hatari ambazo wasipokuwa makini, watajikuta wanatumbukia katika majanga mbalimbali yanayoweza kukiangamiza kizazi cha vijana.

Mfano Ugonjwa wa UKIMWI na Madawa ya Kulevya; ukizingatia ukweli kwamba, Taifa la watu dhaifu kiafya, haliwezi kupambana na umaskini,"alisema Baragomwa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Joseph Mkumbo, alisema changamoto kubwa iliyopo ni kutokuwa na uzio hali ambayo inasababisha baadhi ya wanafunzi hasa wavulana kutoka maeneo mengi kutoendelezwa na kusababisha matokeo kuwa mabaya.

Mkumbo alisema kuwa changamoto nyingine ni upungufu wa meza, uchakavu wa sakafu, milango na madarasa, na malengo ni kuwa na uzio ifikapo Julai mwaka huu ili kudhibiti utoro.Shule hiyo ilianza mwaka 2007 na kidato cha tano kilianza mwaka 2020 na wamehitimu 32.



Baadhi ya Wabunge wakiwa wamesimama Bungeni Dodoma jana kuonyesha kutoa heshima na maombi yao kutokana na kifo cha mbunge mwenzao Irene Ndyamakama kilichotokea juzi Hospitali ya Tumbi Mkoa wa Pwani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wachachamaa mali za ushirika kuchukuliwa

**Na Julieth Mkireri,** MIONO

CHAMA cha Ushirika (AMCOS) Miono Halmashauri ya Chalinze Mkoa wa Pwani kimelalamikia mali za ushirika wao kuchukuliwa bila kufuata utaratibu.

Mwenyekiti wa chama hicho, Iteri Mtewele, aliiomba Ofisi ya Waziri Mkuu kuingilia kati ushirika huo urejeshewe mali zake na anayetaka kuchukua kwa upande wa serikali taratibu zifuatwe.

Alieleza juzi kijijini Miono kuwa mali zinazolalamikiwa awali zilikuwa zinamilikiwa na taasisi ya Darubini na baada ya kuanzishwa vyama vya ushirika Mrajisi aliielekeza Serikali kuwa mali hizo sasa zimilkiwe na Ushirika.

Waraka huo baada ya kufika kwenye vijiji kupitia kwa maofisa ushirika, Serikali ya Kijiji cha Miono ilitoa waraka wa kuwathibitisha kumiliki mali hizo mwaka 2001.

"Sisi baada ya waraka kufika serikali za vijiji tulithibitishwa kumiliki mali zilizokuwa zinamilikiwa na Darubini, baadae vijijini kulikuwa na mgawanyo wa vijiji na viongozi wa kijiji hiki kipya cha Mkwajuni walitwaa mali za ushirika wakidai kuwa mali ni za kwao kwa kuwa zipo kwenye eneo lao bila kufuata utaratibu tumechukua hatua mbalimbali tumeweka kusudio la kwenda mahakamani," alieleza.

Alisema wanachosikitika ni mamlaka za serikali ngazi ya chini kuhujumu ushirika wakati Rais amesema hivi ndio kwa kunyang'anya mali za ushirika bila kufuata taratibu.

"Viongozi wa kijiji kipya mwanzo waliomba kuwaweka wakulima 12 kufanya biashara kwenye eneo la ushirika kupisha ujenzi wa soko jipya, tukakaa nao tukakubaliana na tukaanza malipo tunachoshangaa ilipofika katikati walinyang'anya maeneo hayo, tumewapa siku 90 na zimeisha tunamsubiri mwanasheria wetu kwa hatua zaidi."

Alisema hata eneo lililojengwa ofisi ya Kata ya Miono walijadiliana kabla ya kuanza ujenzi lakini kabla ya kuafikiana walishangazwa na kitendo cha ujenzi kuanza na hata walivyokamilisha hawakuzingatia waliyojadili kwenye kikao cha pamoja.

Alisema wanachoomba kwa Serikali ni kurejeshewa mali hizo kwani sio za mtu ni za ushirika na zikiwepo zinawasaidia.

Shabani Mpwimbwi, mmoja wa wanachama wa ushirika huo, alisema matatizo yalianza baada ya Kijiji cha Miono kugawanywa.

Alisema mbali ya eneo lao kuchukuliwa na Kijiji cha Mkwajuni, lakini pia lipo eneo lao lingine limechukuliwa na Serikali ya Kata ya Miono bila kufuata utaratibu.

"Viongozi wa Mkwajuni waliomba wafanyabiashara wafanye biashara zao kwenye Kijiji cha Miono ambapo walielekezwa kwenye ushirika ambao ndio wamiliki wa eneo hilo... na sisi wanaushirika ndio tuliopima maeneo hayo na walipoanza tulikuwa tunachukua ushuru wa ardhi tunashangaa baadae wamebadilika wakidai ni eneo lao," alisema Shabani.

Alisema viongozi hao wanapojitwalia mali hizo wakiulizwa sababu wanasema ushirika ulishavunjwa, jambo ambalo sio la kweli.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Miono, Sadick Kisagasi, alikiri kuufahamu mgogoro kati ya Ushirika na Serikali ya kata ambao wamejenga ofisi katika eneo la ushirika na Kijiji cha Mkwajuni ambapo wafanyabiashara wao wanafanya shughuli zao kwenye eneo linalodaiwa kuwa ni la ushirika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkwajuni, Heri Nchimbi, alikiri kuwapo kwa mgogoro kati ya Kijiji hicho na ushirika ambao ulianza baada ya mgawanyo wa mali za vijiji.

Bado kuna mkanganyiko kwa baadhi ya viongozi wa ushirika kutokana na kauli zao ambao wengine wanasema walinunua na wengine wakidai ni la kwao wamepewa na Serikali.

Hivi karibuni walikutana na Ofisa ardhi wa wilaya, mwanasheria wa ushirika huo ambao walikubaliana kumaliza suala hilo kupitia vikao wakihusisha viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Diwani wa Miono, Juma Mpwimbwi, alisema eneo hilo si mali ya ushirika na kutokana na mkanganyiko huo Ushirika wanatakiwa kwenda mahakamani ili kuonyesha vielelezo vya umiliki.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Miono, Kilo Charles, alikiri kuufahamu mgogoro huo ambapo alitaka pande zote mbili mlamikiwa na mlalamikaji kila mmoja kufika kwenye kikao kitakachoitishwa wakiwa na vielelezo vya makubaliano yaliyofikiwa awali .

Uongozi wa ushirika huo umesema utatekeleza kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, iliyowataka viongozi kuwachukulia hatua wahujumu ushirika bila kusubiri kazi hiyo kufanywa na mkuu wa mkoa.

## Bodaboda watuhumiwa kulawiti watoto

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAENDESHA pikipiki maarufu kama bodaboda wanatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya kuwalawiti watoto wadogo hususani wanafunzi wa shule za msingi mjini Sumbawanga mkoani Rukwa.

Ofisa wa Dawati la Jinsia katika kituo cha Polisi mjini Sumbawanga, Winni Dilli, alifichua unyama huo wakati wa mdahalo kuhusu uhuru wa kujieleza na maadili ya uandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa ofisi ya mkuu wa wilaya ya Sumbawanga mkoani hapa.

Alisema kwamba kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa walezi na wazazi wa wanafunzi wa shule za msingi kwamba baadhi ya bodaboda wamekuwa na tabia ya kuwabaka na wakati mwingine wakiwaingilia kinyume na maumbile watoto wao wa kiume.

Sio siri watoto wanaumizwa sana tena wakiwa wadogo kabisa wanabakwa na kulawitiwa, hizi taarifa zinaripotiwa katika dawati letu karibu kila siku na tunapofuatilia kwa wanaotuhumiwa mara nyingi wanadai sio wao na tunakosa ushahidi wa kuwatia nguvuni hivyo wanahabari mtusaidie kuelimisha jamii kuhusu suala hili," alisema Winni

Pia alisema kwamba baadhi ya bodaboda hao wanahusishwa na vitendo vya kuwakatisha shule wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambapo hushiriki nao ngono na kuwapa mimba na kuwaoa.

Winni alisema Polisi imekuwa ikifuatilia kesi hizo lakini haipati ushirikiano kutoka kwa wahusika hususani na walezi na wazazi kwa kuwa wengi wao wanakuwa wamewaoza kinyemela watoto hao ambao wengine wanakuwa chini ya miaka 18.

"Ukiona mzazi au mlezi anakuja Polisi kuripoti tukio la mtoto wake kupewa mimba ujue wameshindwa kuelewana sasa anakuja kumtingisha mtuhumiwa kisha Polisi tukianza kufuatilia wanamalizana kimya kimya hivyo kesi inakosa ushahidi na tunashindwa kuipeleka mahakamani," alisema

Hata hivyo, Katibu wa bodaboda mkoa wa Rukwa, Wilson Mwakibete, alikanusha taarifa hizo, na kuongeza kwamba wao wamekuwa wakitoa elimu ya mara kwa mara kwa wenzao wasijihusishe na vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya watoto na wanawake.

"Tatizo kuna watu sio badoboda, lakini ni wamiliki wa pikipiki wanajihusisha na vitendo hivi vya ukatili sasa wananchi wanashindwa kuwatofautisha na sisi wanadai sote ni bodaboda...hawatutendei haki sisi tupo makini sana na tunatoa elimu mara kwa mara na wanachama wetu wanaelewa," alisema.

Awali, Katibu wa Klabu ya waandishi wa Habari ya mkoa wa Rukwa, Sammy Kisika, alisema kwamba mdahalo huo uliodhaminiwa na umoja wa Klabu za waandishi wa habari Tanzania (UTPC) ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano kati yake na international media support (IMS).

Alisema mdahalo huo umeleta pamoja wadau na wanahabari karibu ili kubaini kama jamii ina uhuru wa kujieleza na kuibua changamoto zinazowakabili kwa kushirikiana na waandishi wa habari wa mkoa huo.




Ukurasa 12

Yajue mambo 22 yanayofanywa kiushirika Tanganyika, Zanzibar



Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 26, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

## MIAKA 58 YA MUUNGANO

ASIKUAMBIE MTU KITU...

# Muungano ngome, wainusuru SMZ kuangukia kwa mahaini

IMETIMIA miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tangu ulipoasisiwa mwaka 1964, kwa kipindi cha nusu karne, yamesikika maoni mbalimbali kutoka kwa wanaoamini kuwa Muungano umekuwa wa tija na wale au unaohitaji utizamwe upya.

Uwepo wa Muungamo unatajwa kuwa na manufaa sababu na kimojawapo kikubwa ni kuilinda na kuiepusha SMZ na mikono ya wahaini, ikielezwa kuwa baada ya Mapinduzi ya Januari 1964, kumekuwapo na majaribio zaidi ya 10 ya mtutu wa bunduki ya kuiondoa SMZ madarakani.

Kikwazo pekee kwa mahaini kushindwa kuipindua serikali ni nguzo imara ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, anathibitisha Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa SMZ Dk. Khalid Salum Mohamed.

Ni ushuhuda anaoutoa mjini Zanzibar kwenye kongamano la kujadili na kutathmini miaka 58 ya Jamhuri ya Watu wa Tanzania.

Waziri Mohamed anasema uamuzi wa mataifa mawili ya Tanganyika na Zanzibar kuunda taifa moja haikuwa kazi rahisi na iliwahitaji viongozi wenye uzalendo, umoja na kuona mbali.

Anasema pamoja na kuwepo baadhi ya kasoro, hitilafu na kero za Muungano, anawaondoa wasiwasi Watanzania Bara na Visiwani kuwa masuala hayo yanazungumzika na kusahihishwa.




Makamu wa Pili wa Rais wa SMZ, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza kwenye Kongamano la miaka 58 ya Muungano. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Waziri anasema bado Muungano una tija na faida nyingi kwa pande zote kuliko fikra za kuuvunja kama baadhi ya wanasiasa wanavyokusudia

Dk. Mohamed anasema hati ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar iliposainiwa kulikuwa na mambo 11 hatimaye yakafikia 23 kutokana na sababu za msingi kwa mujibu wa nyakati na mahitaji.

Anasema suala la ulinzi na usalama limepewa kipaumbele ikiwamo kuimarishwa kwa jeshi la ulinzi na vyombo vya usalama.

Anaongeza kuwa kabla ya Muungano kulikuwa na Jeshi la Ukombozi la Zanzibar (JLU) na Jeshi la Tanganyika ila baada ya kuunganishwa likaundwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Aidha, Dk Mohamed anasema kila Mtanzania ana haki ya kuishi mahali popote, kufanya biashara kwa kuwa kuna sarafu moja, hati moja ya kusafiria, benki kuu moja huku gharama zote za uendeshaji zikibebwa na Serikali ya Muungano .

Anasema suala la ulinzi na usalama ni mtambuka na nyeti kwani ustawi wa usalama na amani hutokana na vyombo vinavyosimamia masuala hayo kwa weledi, umakini na uzalendo.

### AMANI IMEDUMU

Katika kongamano hilo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla anasema kipindi cha miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mambo mengi ya msingi yamefanyika ya kimaendeleo kwa Tanzania Bara na Zanzibar yakiwamo kuwepo kwa amani na utulivu.

Anasema hatua hiyo inaonyesha ukomavu na umadhubuti wa Muungano ambao umeleta matunda ambayo wanaendelea kufaidi katika pande zote mbili za Muungano.

Anasema waasisi waliounganisha Tanganyika na Zanzibar hayati Abed Amani Karume na Julius Nyerere, walikuwa na nia thabati ya kuendeleza umoja na udugu pamoja na amani na mshikamano kwa Watanzania

Abdulla anasema fursa nyingi za kiuchumi, kisiasa na kijamii zimepatikana kupitia muungano huo hivyo kuna kila sababu ya kuulinda na kuudumisha.

Anaeleza kuwa maingiliano wa kidamu na kiuchumi yaliyopo baina ya nchi mbili yamesababisha uwepo wa idadi kubwa ya wawekezaji na wafanyabiashara Wazanzibari katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na wafanyabiashara na wawekezaji wa Tanzania Bara waliopo Zanzibar.

Anabainisha kwamba katika kuhakikisha Muungano unaendelea kuimarika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini

INAENDELEA UK.14

NA MWANDISHI WETU, DODOMA

# Yajue mambo 22 yanayofanywa kiushirika Tanganyika, Zanzibar

LEO Aprili 26, Watanzania wanapoadhimisha miaka 58 ya Muungano wa mataifa mawili huru ya Tanganyika na Zanzibar, yaliyounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaendelea kwa amani, umoja na upendo.

Daima wanawakumbuka na kuwaenzi waasisi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume, waliotimiza azma hiyo mwaka 1964.

Pamoja na kuwapo kwa serikali mbili ambazo ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), yapo masuala kadhaa yanayozihusisha pande mbili za Muungano, ikiwamo katiba, sarafu na ushirikiano wa kimataifa.

Yote yanaainishwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoyaorodhesha masuala 22 yanayohusu Muungano.

### KATIBA

Ikumbukwe kuwa kabla ya Muungano, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa huru kila moja akijitegemea. Tanzania Bara, ilikuwa Jamhuri ya Tanganyika iliyoundwa 1962 baada ya uhuru na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar iliyopatikana baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964.

Kabla ya Muungano kila taifa lilikuwa na mamlaka yake (sovereign) ikijumuisha mipaka, katiba, serikali na kujiendesha kiutawala.

Leo kuna katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusika na masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara na Zanzibar inayo katiba yake iliyotungwa mwaka 1984.

Aidha, masuala yote ya Muungano yamewekwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo tangu kutungwa mwaka 1977, imefanyiwa mabadiliko mara 14, lengo likiwa kuiboresha ili iendane na mabadiliko yanayotokea pia kukidhi mahitaji ya wananchi.

### MAMBO YA NJE

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo inayoratibu na kusimamia masuala yote ya kimataifa yaliyo na yasiyo ya Muungano.

Majukumu yake ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, mikataba ya kimataifa pamoja na kuangalia fursa za ushirikiano wa kiuchumi zilizopo na majukumu hayo hutekelezwa pia kwa kushirikisha ofisi za kibalozi.




Viongozi na wahadhiri wakijumuika kwenye mahafali katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA). Elimu ya juu ni eneo linalosimamiwa na Serikali ya Muungano. **PICHA: MTANDAO**

> Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar na Pemba zinahusika, kadhalika hali ya mawasiliano ya simu imeendelea kukua kwa kasi pande zote mbili za Muungano.

Msisitizo ni diplomasia ya uchumi pamoja na kuweka mikakati endelevu ya kuvutia wawekezaji, kukuza utalii ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo.

Aidha, kutokana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ili kukikuza.

Makao Makuu ya Kamisheni yako Zanzibar na pande zote za Muungano zimeshirikishwa kiuwakilishi kwenye masuala muhimu ya kimataifa. Mwongozo kuhusu ushiriki wa SMZ katika masuala mbalimbali ya kimataifa na kikanda umepitishwa na kusambazwa Juni 21, 2019. Umezingatia maeneo ya mikutano ya kimataifa na kikanda, nafasi za masomo ya elimu ya juu na mafunzo mengine nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada na mikopo ya miradi maendeleo.

### ULINZI NA USALAMA

Suala hili limeendelea kutekelezwa kimuungano na vyombo vya ulinzi na usalama vimeendelea kulilinda taifa na kushiriki shughuli za kijamii wakiwamo vijana kutoka pande zote za Muungano kupewa fursa ya kujiunga na vyombo vya ulinzi na usalama kama mafunzo.

### POLISI

Jeshi la Polisi ndilo lenye jukumu la kuhakikisha amani na utulivu vinadumishwa ndani Ya Tanzania na Zanzibar pamoja na kuheshimu sheria na taratibu zilizowekwa.

Polisi inafanya kazi kubwa ya kudumisha amani na kushiriki katika shughuli za kijamii.

### HALI YA HATARI

Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari yako kwa Rais, kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Hali ya Hatari ya 1986 kinampa Mamlaka Rais wa Tanzania kutangaza hali ya hatari na anaweza kukasimu madaraka hayo kwa Rais wa SMZ.

Aidha kwa sheria hiyo, wakuu wa mikoa na wilaya wamepewa madaraka kutangaza hali ya hatari katika maeneo yao.

### URAIA

Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 ndiyo inayotumika, ilitungwa kufuta sheria mbalimbali zilizohusu uraia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata kusababisha mkanganyiko.

Kwa kipindi kirefu tangu kuasisiwa kwa Muungano, utambulisho wa raia wa Tanzania na wasio raia ulikuwa unafanyika kwa kutumia pasi za kusafiria, hati za vizazi na vifo na nyumba kumikumi.

Julai 30 , 2008, Tanzania iliunda Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ikipewa majukumu ya kuhakiki uraia na kusajili taarifa za raia , kutoa vitambulisho na kutengeneza daftari la kudumu la taarifa za utambuzi wa watu zitakazotumiwa na taasisi nyingine.

### UHAMIAJI

Mwaka 1995, sheria zilizokuwa zinasimamia mambo ya uhamiaji, Tanzania Bara na Zanzibar zilifutwa na kutungwa Sheria ya Uhamiaji Namba 7 ya mwaka 1995.

Aidha, sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya uraia ziliunganishwa na kuwa Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995.

Pia, ili kuboresha huduma za pasipoti, serikali ilitunga Sheria ya Kusimamia Utoaji wa Pasipoti na Hati za Kusafiria.

### MIKOPO YA BIASHARA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawasiliana na wahisani kupata mikopo nafuu ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kwa utaratibu uliopo SMZ kwa upande wake inazungumza na wahisani moja kwa moja kwa lengo la kupata misaada kwa kutumia utaratibu uliowekwa.

Mwaka 2009 serikali ilianzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na katika kuimarisha Muungano, kwenye ulingo wa biashara nje na ndani, Ofisi ya TANTRADE Zanzibar imeundwa ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Hatua hiyo ni muhimu katika kuunganisha nguvu ya kuitangaza Tanzania na fursa zake kiuwekezaji, utalii na biashara.

### UTUMISHI

Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, unasimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kwa kuweka utaratibu wa wazi wa ajira katika utumishi wa umma na kuondoa dosari zilizokuwepo.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa ikitoa fursa sawa za ajira kwa wote Bara na Visiwani kwa kuzingatia vigezo.

Kuhusu nafasi za watumishi wa kawaida kwenye taasisi za Muungano, utaratibu wa muda wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika ni asilimia 79 Bara na 21 kwa Zanzibar. Utaratibu huu unatekelezwa kwa mujibu wa Waraka wa Serikali wa Mei 10, 2013.

### KODI YA MAPATO

Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini inasimamiwa na Idara ya Forodha.

Ushuru wa forodha ni kodi inayotozwa kwa bidhaa zote zinazoingizwa nchini na ili kuwa na utaratibu mzuri wa kukusanya na kutumia kodi ya aina hii kwa maendeleo ya Watanzania wote iliamuliwa kuwa Ushuru wa Forodha unaokusanywa Zanzibar uwasilishwe kwenye Mfuko wa Hazina wa SMZ.

### USAFIRISHAJI

Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, majini, posta na simu vimeboreshwa kwa kuwaruhusu watu binafsi kutumia vyombo vya kisasa kusafirisha abiria wa pande zote.

Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar na Pemba zinahusika, kadhalika hali ya mawasiliano ya simu imeendelea kukua kwa kasi pande zote mbili za Muungano.

### FEDHA

Mambo yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo halali pamoja na noti, benki na shughuli zake zote, fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni kabla ya Muungano yalikuwa yanasimamiwa na kila taifa.




Usafirishaji wa shehena na abiria baharini unashirikisha pande zote za Muungano pamoja na wawekezaji binafsi. **PICHA: MTANDAO.**

Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki iliyojumuisha nchi za Yemen, Somalia, Zanzibar, Tanganyika, Kenya na Uganda.

Ilipofika 1964, bodi hiyo ilivunjika na kila nchi kuwa na sarafu yake Tanganyika na Zanzibar zilikubaliana kuwa masuala ya sarafu na sera za fedha kuwa Mambo ya Muungano. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Benki Kuu (BoT) na jukumu la msingi likabaki kuandaa na kutekeleza Sera za Fedha zinazolenga kutunza thamani ya fedha na kudhibiti mfumuko wa bei ili kuchochea ukuaji uchumi.

Muundo wa Benki Kuu una sura ya Muungano, hii ikiwa na maana ya kuwa na watumishi na ofisi pande zote za Muungano.

Aidha, Zanzibar inaendelea kupata gawio la asilimia 4.5 kutokana na faida inayotokana na shughuli za BoT.

### LESENI VIWANDA, TAKWIMU

Shughuli za leseni na takwimu za viwanda zipo chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na chombo cha utekelezaji ni Mrajisi wa Viwanda na Bodi ya Kutoa Leseni za Viwanda.

Mrajisi wa Viwanda na Bodi ya utoaji wa Leseni za Viwanda wanashirikiana na Naibu Msajili wa Viwanda Zanzibar.

### ELIMU YA JUU

Elimu ya juu ilikuwa mojawapo ya maeneo yaliyopewa kipaumbele baada ya Muungano, kabla ya hapo, Zanzibar haikuwa na chuo kikuu wakati Tanganyika ilikuwa na Chuo Kikuu Dar es Salaam pekee kilichoanzishwa Oktoba 25, 1961 kikiwa chuo kishiriki cha Chuo Kikuu cha London, Uingereza.

Mwaka 1963, chuo kishiriki cha Dar es Salaam kilijiunga na vyuo vikuu Vishiriki vya Makerere na Nairobi na kuunda Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki.

Kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wataalamu wazalendo wa fani mbalimbali na kujenga uwezo wa ndani kielimu, mwaka 1967 Serikali iliamua kuingiza suala la Elimu ya Juu katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Julai 1, 1970 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu kamili baada ya kukivunja Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki.

Kwa upande wa Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kilianzishwa Septemba, 2001.

Mwaka 2005, serikali ilianzisha Tume ya Vyuo Vikuu ili kudhibiti ubora wa elimu ya juu kwa kusimamia ubora wa mazingira ya kufundishia, majengo, mitaala, walimu na taratibu za mitihani.

Tangu kuanzishwa kwake, udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu kutoka pande zote za Muungano hufanyika kwa kuzingatia vigezo muhimu vinavyowawezesha kusoma katika vyuo kote nchini.

### MALIASILI

Mafuta ghafi na yaliyochujwa yakiwamo petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na gesi asilia suala hili liliingizwa kwenye mambo ya Muungano mwaka 1968.

Kwa upande wa Tanzania Bara, suala hili linasimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) wakati Zanzibar, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Hoja ya namna ya kugawana mapato ya mafuta na gesi asilia itakapopatikana, serikali baada ya kujadiliana, zilimtumia mshauri mwelekezi AUPEC kutoka Uingereza kushauri kitaalam mgawanyo huo. AUPEC ilikamilisha kazi hiyo na kuwasilisha mapendekezo kwa serikali zote.

Sheria zimetungwa ikiwemo Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 ya SMT ambayo ilifuta sheria ya zamani, Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta Sura ya 328 na kuipa Zanzibar Mamlaka ya kuanzisha chombo au vyombo vya kusimamia masuala ya mafuta na gesi asilia kwa kutumia Sheria ya Zanzibar. Hivyo, Zanzibar ilitunga sheria yake ya Mafuta na Gesi Asilia mwaka 2016.

### KUSIMAMIA MITIHANI

Baraza la Taifa la Mitihani la Taifa (NECTA) linahusika na usimamizi wa mitihani chombo hiki kipo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu likiwa kutunga na kusahihisha mitihani kwa pande mbili za Muungano isipokuwa kwa mitihani ya kidato cha tatu ambayo hutungwa na SMZ.

NECTA inaendeshwa na Bodi ya Wakurugenzi yenye wajumbe kutoka pande zote, aidha, huajiri watumishi kutoka pande zote.

### SEKTA YA ANGA

Usafiri na usafirishaji wa anga, ni sekta ambayo inaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuuboresha uwanja wa ndege wa Zanzibar, kufungua ofisi ndogo ya msaidizi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Zanzibar na kuruhusu mashirika ya watu binafsi kuendesha biashara ya usafiri na usafirishaji. Aidha, usimamizi, udhibiti na Sera ya Usafiri na Usafirishaji wa Anga vimeendelea kusimamiwa na kuratibiwa katika sura ya Muungano.

### UTAFITI

Ni eneo linalosimamiwa na kuratibiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) liyoanzishwa mwaka 1986 ambayo hutumika pia Zanzibar. Wajumbe wa Bodi ya COSTEC hutoka Bara na Zanzibar.

### HALI YA HEWA

Utabiri wa Hali ya Hewa husimamiwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa chini ya Wizara ya Miundombinu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

### TAKWIMU

Kila upande una sheria na idara ya kusimamia takwimu, hata hivyo wakati wa kuhesabu watu au sensaa idara hizo mbili hufanyakazi pamoja.

### MAHAKAMA YA RUFANI

Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano inasikiliza kesi zinazohusu masuala yote isipokuwa kesi zinazotokana na masuala ya dini ya Kiislamu zilizoamuliwa kwa upande wa Zanzibar. Mahakama ya Rufani ina vituo Dar es Salaam (Makao Makuu); Mwanza,Dodoma, Arusha, Zanzibar, Mbeya na Tanga.

### KUANDIKISHA VYAMA

Uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana na navyo ni suala la Muungano.

Kufuatia uamuzi wa serikali wa kuruhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992 na kutungwa kwa Sheria ya Vyama vya Siasa, sura 258, uandikishaji wa vyama vya siasa uliorodheshwa kwenye mambo ya Muungano.

Hadi kufikia mwaka 2020 Vyama 21 vimesajiliwa na vimeshiriki kikamilifu katika masuala mbalimbali ya kisiasa nchini.

Aidha, Ofisi ya Msajili wa Vyama imefungua tawi la Ofisi zake Zanzibar ili kuongeza ufanisi katika kuhudumia vyama vya siasa pande zote mbili za Muungano.

Hivyo, usimamiaji makini wa utekelezaji wa mambo ya Muungano unathibitishwa na mafanikio yaliyopatikana yakijumuisha kuimarika kwa utaifa na umoja, amani na utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zote mbili.

Pia, utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa mujibu wa katiba na sheria na yale yasiyo ya Muungano unakwenda sanjari na mipango, sera, programu na mikakati ya maendeleo ambayo serikali zote mbili zilijiwekea.

# Muungano ngome, wainusuru SMZ kuangukia kwa mahaini

INATOKA UK.11

ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, wanasimamia makubaliano ya kuondoa hoja 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi.

**TANZANIA INAIGWA**

Mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, akizungumza kwenye jukwaa hilo, anasema Muungano wa Tanzania ni wakuigwa duniani kwa sababu zipo nchi ambazo zilijaribu kuungana lakini zilishindwa kutokana na vikwazo mbalimbali.

Anasema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni wa kipekee na wenye faida na mafanikio makubwa na hadi sasa hakuna mtu aliyeupinga duniani.

"Wapo watu kwenye mitandao ya kijamii ambao wanaubeza Muungano wetu lakini hakuna hata mmoja mwenye heshima zake aliyekwenda Umoja wa Mataifa (UN) na kushtaki kuwa unashida na haukufuata utaratibu", anasema.

**MUUNDO UNADUMISHA**

Mwanasiasa mkongwe Steven Wassira, akijumuika kwenye kongamano hilo mjini Zanzibar, anasema Muungano wa serikali mbili uliopo sasa ndiyo imara ambao unauhakikishia kuwa utaendelea kuwa wa kudumu.

Kwa msimamo huo anatofautiana na baadhi ya wanaotaka serikali tatu ambao anauita muundo utakaovunja Muungano.

Wassira anasema Muungano wa serikali mbili unaihakikishia Zanzibar kuwa na utawala wake na wananchi wake kuendelea kufuata mila, utamaduni ikiwa ni sehemu ya utambulisho wake.

Anasema waasisi wa Muungano Mwalimu Julius Nyerere, pamoja na Shekhe Abeid Amani Karume, walikuja na wazo la kuwepo kwa Muungano wa Serikali mbili ambao unaihakikishia Zanzibar kuendelea kuwepo katika uongozi wake za serikali bila ya kupoteza utambulisho wake wenye utamaduni wa asili.

Anasema wapo watu wanaodai kuwepo kwa serikali tatu ambazo hazina maslahi na uhai wa Muungano uliopo ambao hatimaye utakufa.

"Vijana ni muhimu kufahamu historia ya Muungano ambayo kadri siku zinavyokwenda wapo watu wamekuwa wakifanya upotoshaji mkubwa ikiwemo kuonyesha kwamba Muungano huu hauna faida kwa Zanzibar"anasema.

Kwa mfano anasema hata kabla ya Mapinduzi yapo makabila ambayo yalikuwepo Zanzibar kama Wamakonde,Wanyamwezi pamoja na Waluguru na Wamanyema huku wakiwapo watu waliofika mapema kutoka Bara wakitokea katika visiwa vidogo kama Mafia na Kilwa.

Anasema makabila hayo yalikuwa na mchango mkubwa katika Mapinduzi ya Januari 12, 1964 na kuendelea kuwepo Zanzibar yakidumisha maingiliano na kuchanganya damu.



Waasisi wa Muungano , Abeid Amani Karume (kushoto) na Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MAKTABA**

## WANENAVYO MALENGA

### MUDA KUJITATHMINI

Jumuiya hii yetu, au twadai ni yetu?
Ya kwamba bajeti yetu, sehemu si jasho letu,
Tunategemea watu, walipie mambo yetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Hao mawaziri wetu, na wawakilishi wetu,
Kusema bajeti yetu, kwa sehemu siyo yetu,
Kwamba marafiki zetu, ndio egemeo letu,
Afrika mashariki, muda kujitathmini.

Ingekuwa bora kwetu, kubajeti mambo yetu,
Fedha zitokee kwetu, kwa huu umoja wetu,
Tukifanya mambo yetu, mgeni asiwe kwetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Zaidi theluthi yetu, bajeti siyo ya kwetu,
Hivyo hata mambo yetu, theluthi siyo ya kwetu,
Atupaye pesa kwetu, ataona mambo yetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Nchi saba huku kwetu, kwenye Jumuiya yetu,
Tuchange michango yetu, tujenge umoja wetu,
Hao marafiki zetu, waongeze nguvu kwetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Dola milioni zetu, tisini bajeti yetu,
Theluthi siyo za kwetu, ni za washirika wetu,
Hatuwezi peke yetu, kuendesha chombo chetu?
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Arusha makao yetu, huko kuna Bunge letu,
Jadili bajeti yetu, kujitegemea kwetu,
Misaada ije kwetu, nyongeza ya nguvu zetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Wakitoa pesa kwetu, twakosa uhuru wetu,
Watataka mambo yetu, mazuri kwao si kwetu,
Sababu si pesa zetu, huo ni unyonge kwetu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

Uhuru tuwe na vyetu, tokana na jasho letu,
Tuyapange mambo yetu, kwa huu undugu wetu,
Tufike mkono wetu, ufikapo pale petu,
Afrika Mashariki, muda kujitathmini.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### JUKUMU LA KILA SIKU

Bora kuotea jua, mwili unaufungua,
Ulikuwa unajua, au kama hukujua,
Afya ya mwili ni jua, mwili linaufungua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Mwili tunavyoujua, kupumzika wajua,
Vile vinavyougua, kutumika kwapungua,
Kesho likitoka jua, ukurasa wafungua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Mazoezi tunajua, viungo yanafungua,
Muda tukiuchukua, mengi tunayatatua,
Ni sawa nguo kufua, na vizuri kukamua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Chakula tunakijua, njaa zetu chatatua,
Anza kinywa kufungua, lishe njema kutambua,
Si kufukuafukua, kila kitu wakijua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Vyakula kufukunyua, eti kwamba watanua,
Magonjwa unachukua, bila ya wewe kujua,
Usiseme sikujua, sasa ndio unajua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Kujiamini tambua, hata mwili unajua,
Sawa ua kuchanua, baadaye kuchavua,
Woga mwili wasumbua, na magonjwa kununua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Hawa si wa kununua, ni jinsi ya kuwajua,
Si wa hewa kuchafua, ubaki wapigwa jua,
Endapo ukiwajua, maisha wayafungua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Marafiki twawajua, sura zao wafunua,
Na vizuri watujua, pendo si la kuchagua,
Hao chaguachagua, utazidi kutanua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Kujifanya unajua, peke yako watanua,
Iwe mvua au jua, hutaki mtu kujua,
Mwisho kuja kung'amua, maisha meshakamua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

Mungu kama wamjua, imani waichukua,
Mengi atakufungua, changamoto kutatua,
Maishani kuungua, huwezi ukakujua,
Kujenga afya ya mwili, jukumu la kila siku.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Serikali yawaahidi fursa watu wenye mahitaji maalum

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Athony Mavunde, amesema serikali itaendelea kujali makundi ya watu wenye mahitaji maalumu kwa kuwawezesha kwa namna mbalimbali.

Miongoni mwa uwezeshaji huo ni wa kielimu, afya na kiuchumi.

Mavunde alitoa ahadi hiyo katika hafla ya futari ya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani iliyofanyika katika Msikiti wa Gadafi iliyoandaliwa na Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA) Wilaya ya Dodoma.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa kuyafikia makundi ya watu wenye uhitaji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakichangia misaada yenye tija kama elimu, afya na kwenye maisha yao ya kila siku.

Alisema kutokana na juhudi ambazo zimefanywa na Jumuiya hiyo ni mategemeo yake taasisi zingine zitaungana kuhakikisha makundi hayo yanapata mahitaji yao.

"Hapa tuna wanafunzi hao wanaolelewa na BAKWATA kupitia idara mbalimbali za kiislamu,wanatakiwa kupatiwa misaada mbalimbali kuwawezesha kuondokana na changamoto walizonazo, hivyo sisi kama serikali tutaendelea kuwatazama na kutatua mahitaji waliyonayo,"alisema.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, aliwaomba wadau kutoka taasisi mbalimbali za kidini na serikali kujitokeza kusaidia jamii ambazo hazina uwezo wa kimaisha.

Shekhe Rajabu, alisema bado kuna changamoto kwenye makundi hayo yasiyojiweza,hivyo ni wajibu kwa taasisi hizo kujitoa ili watu hao waweze kupata haki zao za msingi kama vile afya, chakula, mavazi na elimu.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Filipi Yimbi, aliipongeza Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania wilaya ya Dodoma kwa kuwakumbuka watoto yatima na wajane.

# Hekta 580 za mahindi na alizeti zaliwa na ng'ombe

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

HEKA 580 za mahindi na alizeti katika kitongoji cha Wali wilayani Chamwino zimeliwa na ng'ombe baada ya jamii ya wafugaji kuingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima. Tukio hilo inadaiwa ni sehemu ya mgogoro kati ya wakulima na wafugaji ambao wamekuwa wakigombania mpaka na kata jirani ya Chitego wilayani Kongwa kwa zaidi ya miaka 18.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alifanya ziara juzi ya kutembelea mashamba hayo na kuzungumza na pande zote mbili ili kupata muafaka.

Akizungumza na wananchi wa kitongoji cha Wali, alisema serikali itahakikisha inalifanyia kazi suala hilo na halitajirudia tena.

"Hichi ambacho kimefanywa na wafugaji hakistahili kufumbiwa macho kwani hata kama mtu ana makosa huwezi kabisa kuingiza mifugo katika shamba la mtu na kulisha mazao yake yote" alisema.

Aidha, aliuagiza uogozi wa wilaya ya Chamwino na Kongwa kukaa pamoja na kufanya tathmini ya uharibifu wa mazao hayo uliofanywa na wafugaji.

"Ifanyike tathmini ili kubaini kuwa wakulima kiasi ambacho walikuwa wamewekeza na kwa yeyote aliyehusika na kukamatwa hatua kali za kisheria zichukuliwa ikiwamo kulipa fidia kwa kiasi ambacho wakulima walitarajia kupata baada ya kuvuna.

"Katika wakati wote nitakapokuwa Dodoma jambo hili mimi sitaruhusu kutokea kwani ni ujinga... mtu kulisha mazao ya mtu eti tuu kwa sababu ya mgogoro wa mpaka hakikisheni kila aliyehusika analipa kwa mujibu wa sheria,"alisema Mtaka.

Aliwahakikishia wakulima ambao mashamba yao yameliwa na mifugo kutokuwa na wasiwasi kwani mkoa utahakikisha kila mmoja wao anapata haki yake.

"Pia nawataka wakurugenzi mrudi kazini na mkae pamoja ili timu ya wataalamu wa ardhi ije haraka na kufanya kazi yake na kuondoa kero hii ya mgogoro wa wakulima na wafugaji,"alisema.

Vilevile, aliwataka wafugaji kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwani ni kinyume cha sheria za nchi.

"Kama mfugaji unataka kuendelea kuwa kitega uchumi cha wakulima basi wakulima wataendelea kulima na wewe endelea kuingiza mifugo yako ili kila mwaka uwe unawalipa,"alisema.

Aliwataka wafugaji badala ya kuendelea kugombania ardhi ya serikali wahakikishe kuwa wanapima kwanza waliyonayo ili kuimiliki kihalali.

"Hichi mnachokifanya ni sawa na kugombania hawala baa kwani hii ni ardhi ya serikali pimeni kwanza ya kwenu ili muimiliki kihalali vinginevyo hata hiyo mnaweza kuikosa"alisisitiza Mtaka

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alisema wameshakamata ng'ombe zaidi ya 300 pamoja na wafugaji ambao walihusika katika kulisha mashamba ya wakulima na hatua nyingine za kisheria zinaendelea.



Daktari Bingwa wa upasuaji wa mdomo wazi kutoka Hospitali ya Dodoma, Athanus Masele akiongoza jopo la madaktari katika zoezi la upasuaji wa mdomo wazi kwa watoto katika Hospitali ya TPC iliyopo wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro ikiwa ni zoezi lililofadhiliwa na Taasisi ya The Same Qulities Foundation. **PICHA: MARY MOSHA**

# Rais Samia awakuna wajasiriamali wanawake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wanawake jijini Dodoma wamemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wadogo yanayowezesha kufanya kazi zao kwa tija na kujiletea maendeleo.

Wito huo ulitolewa jijini Dodoma wakati wa ziara ya Menejimenti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ikiongozwa na Katibu Mkuu, Dk. Zainab Chaula na Naibu wake, Amon Mpanju.

Akizungumza na viongozi hao, mjasiriamali anayejishughulisha na uchakataji wa bidhaa za plastiki, Aziza Abdi Hassir, alisema aliamua kufanya shughuli hiyo kwa sababu ya kutaka kujiajiri na kufanya kazi ambayo itasaidia watu wengine.

Aliongeza kuwa kazi hiyo alianza mwaka 2009 kwa kuanzisha kampuni ikiwamo dampo na alijifunza kutoka kwa ndugu yake mkoani Dar es Salaam kuanza kupelekea chupa na bidhaa za plastiki kwa wanunuzi katika viwanda vikubwa.

Alisema kwa sasa ana uwezo wa kupeleka tani 90 za chupa na bidhaa za plastiki katika viwanda ikiwamo chupa zenye soko mkoani Dar es Salaam na plastiki zenye soko mkoani Dodoma katika viwanda mbalimbali.

Aidha alisema kwa sasa ana uwezo kuuza mzigo wa Sh milioni 16 kutokana mzigo wa tani 20 na pia wakiwa na uwezo wa kuzalisha tani 90 kwa wiki inayowawezesha kupata faida ya milioni 10 kwa wiki kutokana na biashara hiyo.

"Mwanzoni hata mume wangu aliona aibu na kuwaza kwanini nifanye biashara hii ya chupa, ila baada ya kuona mafanikio ameona faida yake na yeye sasa ndio amekuwa mfanyakazi mkubwa zaidi ya mimi," alisema Aziza.

Hadija Zuberi aliiomba serikali kuwatazama wajasiriamali kwa jicho la tatu hasa wanaojishughulisha na biashara ya chupa, bidhaa za plastiki na taka ngumu kwa kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa ili kupata soko kubwa la kupeleka malighafi zaidi na kuongeza ajira na kipato.

Dk. Chaula alisema nia ya serikali ni kuyawezesha makundi maalum wakiwamo wajasariamali kwa kuwawekea mazingira wezeshi.

"Tumekuja hapa kwa lengo la kujifunza na timu nzima ya menejimenti ya wizara pamoja na Naibu Katibu Mkuu wangu ... lengo tujue changamoto zinazowakabili wajasiriamali na kuweka mikakati thabiti ya kusaidiana na wizara za kisekta katika kutatua changamoto hizo," alisema Dk. Chaula. Mpanju aliwapongeza wanawake hao kwa kuanzisha biashara hizo na kuwasaidia vijana kupata ajira zinazowasaidia kuendesha familia zao, hivyo kuwezesha watu wengi zaidi kupitia biashara hiyo.

Aliongeza kuwa wizara imechukua maombi na changamoto zao na itahakikisha kushirikiana na Wizara za kisekta, kuzitatua kwa manufaa ya wajasiriamali katika kuendeleza shughuli zao.





# Biashara vyuma chakavu sasa yapigwa marufuku

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI ya Wilaya ya Mbeya imepiga marufuku biashara ya vyuma chakavu baada ya kubaini kuwapo kwa kundi kubwa la watoto wa mitaani kujiingiza katika biashara hiyo na kuhusika katika matukio ya uhalifu, ulawiti, ngono, ulevi na madawa ya kulevya.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, wakati akieleza mikakati ya serikali kukabiliana na wimbi la watoto wa mitaani wanaotoka mikoa mbalimbali kufanya biashara ya vyuma chakavu mkoani Mbeya na kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu.

"Kumeibuka kundi kubwa la watoto mitaani wengi wao sio wazaliwa wa Mbeya wanatoka mikoa mbalimbali nchini licha ya kujihusisha na biashara ya vyuma chakavu, lakini pia wanajihusisha na uhalifu, ulawiti, ngono zisizo salama, matumizi ya pombe na madawa ya kulevya ambao wanaishi kwa kuokota na kuuza vyuma chakavu," alisema Dk. Chuachua.

Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Wilaya ya Mbeya imepiga marufuku biashara hiyo kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuagiza watoto wote warejeshwe makwao.

Alisema katika kufanikisha suala hilo, atakutana na wakurugenzi wa halmashauri pamoja na wadau wa malezi na makuzi kuona namna bora ya kupata taarifa za watoto watakaobainika kutoka mikoani na kufanya mawasiliano na familia zao na kuwarejesha kwa utaratibu maalum," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alikiri kuwapo kwa kundi kubwa la watoto hao na kwamba kwa mwaka jana zaidi ya 200 walitambuliwa na baadhi walirejeshwa makwao na wengine kupelekwa katika vyuo vya ufundi stadi.

Alisema licha ya kuwarejesha makwao, mwaka huu wamekuwa wengi na miongoni mwa mikakati ni kupiga marufuku biashara hiyo pamoja na kuagiza kurejeshwa makwao.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali Sauti ya Mama Afrika (Samofa), Thabitha Bughali, alisema kwa Mkoa wa Mbeya kuna tatizo kubwa la ajira kwa watoto, lakini alishauri serikali kuona namna ya kujenga kituo cha malezi na makuzi.

Alisema mbali na kundi hilo la watoto wa mitaani pia kuna wazee wanaoishi maisha duni ambao wametelekezwa na familia zao na kugeuka ombaomba nao pia wanapaswa kuangaliwa na serikali kushirikiana na wadau.



Mchimbaji wa madini ya dhahabu Abdallah Moses anayefanya shughuli zake katika Mgodi wa Mlima Elizabeth, ulioko eneo la Saza Mkwajuni wilayani Songwe akiendelea na shughuli za kutafuta madini kwenye mojawapo ya mashimo waliyoyachimba juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Bajaji sasa nauli rasmi zatangazwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UMOJA wa Madereva Bajaji Jiji la Mbeya umetangaza rasmi kupandisha nauli kutoka Sh. 500 mpaka 700 kwa kila kituo kuanzia juzi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa umoja huo, Feso Mwasimba alisema, wamefikia uamuzi huo sio kwa sababu ya kupanda kwa bei ya mafuta bali ni kwa sababu nauli ya Sh. 500 imedumu kwa kipindi cha miaka tisa sasa.

Alifafanua kuwa bei hiyo sasa itatumika pia kwa wanafunzi wa shule za sekondari kutoka Sh. 200 hadi 300 huku mwanafunzi wa shule ya msingi akilipa Sh 200.

"Bajaji ni chombo cha kukodiwa na abiria sio sawa na daladala ambazo wanapangiwa nauli na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) pia, madereva bajaji wanalalamikia sana nauli ya Sh. 500 kila mwaka pasipo kupandishwa," alisema Mwasimba.

Alisema kutokana na malalamiko hayo, Aprili 21, 2022 walikaa kikao na kupitisha uamuzi huo na kutoa matangazo kwa kila bajaji kubandika nauli mpya ili abiria wazione na kuondoa sintofahamu kuanzia Aprili 25 inapoanza nauli mpya.

Dereva bajaji anayefanya safari za Kabwe kwenda Iyunga, Yasim Ally, alisema kuwa kiwango cha nauli kuwa 700 ni kidogo walitarajia ingefika Sh. 1,000 kwa kila abiria ili kufidia gharama za mafuta na kupata malengo ya wamiliki wa bajaji.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) Kanda ya Nyanda za Juu, Denis Daudi alisema kwa sasa hana taarifa ya uamuzi huo wa usafiri wa bajaji kupandisha nauli kutoka Sh. 500 mpaka 700.

Alisema kuwa atafanya mawasiliano na uongozi wa bajaji mkoa huku wakiendelea kusubiri bei elekezi ya serikali ya kupanda kwa nauli kwa usafiri wa umma na bajaji nchini.

# Sababu za kuporomoka soko la parachichi zatajwa

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

KUPOROMOKA kwa soko la parachichi zinazozalishwa wilayani Rungwe, imedaiwa ni kutokana na kuwapo kwa vita ya kiuchumi baina ya nchi ya Russia na Ukraine kwa sababu ya meli zilizokuwa zikitumika kusafirisha shehena za mizigo kusitisha safari.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya, Dk. Vicent Anney, baada ya kufanya ziara ya mashamba ya wakulima, vituo vya ununuzi na kuzungumza na wawekezaji wa Kampuni ya Kuza Afrika inayojihusisha na kilimo cha parachichi na usafirishaji nje ya nchi hususani, Dubai, India na Russia.

Akizungumza mbele ya Mkuu wa Wilaya, Meneja Rasilimali watu wa Kampuni ya Kuza Afrika, Noel Kabuje, alisema tangu kuanza kwa vita hiyo usafirishaji wa shehena za parachichi umepungua kutoka wastani wa tani 100 mpaka 20 kwa wiki sawa na kontena saba mpaka nane za shehena ya mzigo.

Alisema kuwa hali hiyo imewaathiri kwa kiwango kikubwa na sasa wanategemea masoko kwa wateja wachache ambao wananunua kwa oda na kusafirishiwa kwa njia ya ndege.

"Mkuu wa wilaya kwa sasa vita ya Urusi imeathiri biashara ya parachichi, kutokana kwa sababu usafiri mkubwa wa bidhaa hizo kimataifa ni meli ambazo asilimia kubwa zinamilikiwa na raia wa nchi hiyo ambazo baada ya kuibuka machafuko zimesitisha safari kusababisha kuwa mwiba kwetu wasafirishaji," alisema Kabuje.

Mkuu wa wilaya, Dk. Vicent Anney, alisema kuwa amelazimika kuingia mashambani kwa wakulima na kukagua vituo vya mauzo ya parachichi baada ya kusikia taarifa za malalamiko ya wakulima kudai matunda kuozea mashambani kwa kukosa masoko.

"Nimeona hali halisi ya zao la parachichi kwa wakulima nimeona uzalishaji umekuwa mkubwa masoko hakuna na pia kwa wenzetu wawekezaji wa makampuni kushindwa kusafirisha sababu ikiwa ni vita vya Urusi na Ukraine ambavyo vimechochea usafiri wa meli kukwama," alisema Dk. Anney.

Alisema kutokana na vita hivyo, serikali inatafuta mwarobaini wa kuona tatizo hilo linatafutiwa ufumbuzi kwa kuangalia milango mingine ya soko ya ndani inafunguka sambamba na kuthibiti madalali wa kati ambao wana wakandamiza wakulima kwa kujipangia bei.

Mkulima ambaye pia mjumbe wa bodi ya Chama cha Ushirika cha Wakulima wa parachichi wilaya ya Rungwe (Uwamaru), Christopher Mwene alisema hali hiyo imechochea kundi kubwa la madalali kuingia mashambani na kununua parachichi kwa bei ya Sh. 600 kwa kilo badala ya bei elekezi ya serikali ya Sh. 1,600.

Alisema kutokana na tatizo hilo, wanaomba serikali iwafuatilie na kuwachukulia hatua madalali wanaoingia mashambani kwa madai hawana leseni halali za ununuzi na wanakwepa kulipia mapato serikalini.






Katibu wa Baraza la wawakilishi Raya Issa Mselem (kati) akizungumza na waandishi wa habari ambao hawapo pichani kuhusu kikao cha baraza hilo kitakachoanza kesho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Bajeti Kuu Serikali ya Mapinduzi kusomwa Juni 6

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa saba wa baraza la kumi la Wawakilishi unatarajiwa kuanza Aprili 27, mwaka huu ukiwa na bajeti kuu ya Serikali ya Zanzibar ya mwaka 2022/2023.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Baraza hilo Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar, Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Mselem, alisema mkutano huo utajumuisha shughuli mbalimbali za serikali ikiwamo maswali na majibu 185.

Alisema pia miswada miwili ya serikali itawasilishwa na kujadiliwa ikiwamo mswada wa sheria ya fedha na mswada wa sheria ya kudhibiti matumizi ya serikali kwa mwaka 2022/2023.

Alisema bajeti kuu ya serikali itasomwa Juni 6, mwaka huu na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya.

Alisema kuwa Baraza la wawakilishi linaendelea na utaratibu wa baraza mtandaoni ili kupunguza matumizi ya karatasi.

"Bado hatujafanya tathmini rasmi kuhusu matumizi ya baraza mtandaoni, lakini mfumo huu umesaidia sana kudhibiti mapato, lakini pia kuhifadhi mazingira," alisema Katibu huyo.

# Makandarasi watakiwa kuharakisha ujenzi barabara Chakechake-Wete

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKANDARASI wanaojenga Barabara ya Chake- Wete Pemba yenye urefu wa kilomita 22.1 wametakiwa kufanya kazi kwa kasi ili barabara hiyo ikamilike kwa wakati.

Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, mawasiliano na Uchukuzi, Juma Makungu Juma, aliyasema hayo wakati alipokua katika ziara ya kuzikagua barabara zinazojengwa kisiwani Pemba pamoja na minara ya mawasiliano. Waziri Juma alisema kuwa, barabara hiyo ni tegemeo la wananchi ambayo baada ya kukamilika itasaidia kuunganisha mawasiliano baina ya watu kutoka pande zote za mikoa ya Pemba.

Alisema serikali tayari imejipanga kutatua changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa kazi hiyo, na kampuni iliyopewa dhamana ya kufanya ujenzi katika barabara hiyo inatakiwa kuzingatia muda uliopangwa ili wamalize kazi kwa wakati uliopangwa.

Naye Meneja mradi anayesimamia ujenzi wa barabara hiyo kutoka kampuni ya MECO, Vedesto Tega, alisema tayari kampuni yao imefanikiwa kusafisha eneo la kilomita tatu ikiwamo kukata miti pamoja na kuondoa vizuwizi katika barabara hiyo.

Pia, aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao wataguswa na mradi huo ili kuokoa muda wakati wakiwa tayari kuendelea na kazi katika maeneo mengine.

Wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya maeneo huru ya uwekezaji Micheweni Pemba ambayo barabara hiyo imeshaanza kuwekwa lami, Naibu Waziri Juma alimtaka Mkurugenzi wa Wakala wa Barabara kuharakisha kazi ya uwekaji wa lami na serikali imekusudia kukaribisha wawekezaji kupitia eneo hilo. Katika ziara hiyo, Naibu Waziri huyo pia alitembelea barabara ya Chimba, Finya - Kicha, Maambani pamoja na Bandari ya Shumba Mjini, kisiwani humo.

Akiwa katika barabara ya Maambani ambayo inajengwa kwa Mfuko wa Mwakilishi, wakazi wa eno hilo walimuomba kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha kifusi kutokana na kukabiliwa na changamoto kipindi ambacho wanahitaji kuwapeleka wagonjwa hospitali wakiwamo wajawazito wakati wa kujifungua.

Naibu waziri huyo pia alitembelea ujenzi wa minara mbalimbali ya mawasiliano kisiwani Pemba ikiwamo mnara unaojengwa Msuka, Kangagani pamoja na kuukagua mnara wa Kigomasha uliopo Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba.

# Masoud awapa mwongozo vijana shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, amesema vijana Zanzibar wanawajibika kusoma kwa dhamira ya kufikia mwelekeo wa mabadiliko ya dunia katika maendeleo ya sayansi na teknolojia na sio kukamilisha elimu za vyuo vikuu.

Aliyasema hayo Shule ya Sekondari ya Fedelcastro Pemba, alipozungunza na walimu na wanafunzi wa shule hiyo alipoitembelea. Alisema dunia ya sasa ni ya mahitaji ya matumizi makubwa ya elimu ya sayansi na teknolojia inayotokana na maarifa ya kitaaluma na kwamba vijana wa Zanzibar ni lazima wawe na jitihada za kupata elimu na kutumia maarifa katika mabadiliko ya dunia yanayohitajika.

Alisema kuwa maendeleo hayo yamefikiwa kutokana na jitihada za kusoma na kutumia maarifa ya elimu jambo linalowezekana iwapo vijana watafanya jitihada za kutafuta elimu inayohitajika katika maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia.

Alisema maendeleo hayo hayawahusu wazungu pekee, lakini kila mmoja ana uwezo wa kujitahidi na kufikia ubingwa wa utaalamu katika fani mbalimbali ukiwamo, urubani, uhandisi, udaktari na mengine mengi na kusaidia maendeleo ya taifa.

Othman alisema hakuna ukomo wa kupata elimu kwa mwanadamu, lakini jambo muhimu linalohitajika ni juhudi ya kila mmoja na kuweka dhamira ya kufikia safari ya malengo ya kutafuta elimu aliyoyaweka na kutarajia maendeleo.

Aliwataka vijana kujitambua na kuona kwamba kwa jitihada kila mmoja ana uwezo kama alionao mtu mwingine wa kuwa mtaalamu bingwa na aliyebobea baada ya kuweka malengo na matarajio. Aliwataka vijana wasibabaike kwa kuingia kidato cha nne na sita na badala yake waitumie fursa hiyo kama ni ufunguo wa kuongeza jitihada za kusonga mbele zaidi katika safari ya kutafuta upeo wa elimu zaidi.

Kwa upande wa serikali alisema inakusudia kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu na tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeagizwa kuandaa na kuwasilisha serikalini mpango madhubuti wa mageuzi muhimu katika sekta elimu ili kwenda sambamba na mahitaji ya sasa katika kufikia maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Vile vile, alisema mpango huo wa mageuzi utahusisha pia nyenzo za kisasa, vifaa na matumizi ya rasilimali fedha na watu ili uweze kukidhi dhamira ya mageuzi inayohitajika na serikali kwa maendeleo ya nchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Msoud, alisema jitihada zinazofanywa na walimu wa Shule ya Fedelcastro zimewezesha shule hiyo kupata matokeo mazuri katika matokeo ya mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne na sita.

Alisema, katika kuunga mkono juhudi hizo serikali inaendelea na ujenzi wa madarasa mapya katika shule mbalimbali ili kupunguza wingi wa wanafunzi madarasani jambo ambalo litasaidia kuongeza mafanikio katika sekta hiyo ya elimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**

**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi............79/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ERNEST APPELES SHEWALI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**

**YALIYOLETWA NA: CARLOS ERNEST SHEWALI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28/4/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo 21/4/2022**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IMANI BRIGHTON MWAKASAGULE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya MITSUBISHI FUSO yenye usajili namba **T612 DFU,** CHASSIS NAMBA **KF627G530018,** ENGINE NAMBA: **6D25654565.** Kwa yeyote atakaeiona atoe tarifa kituo cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/161687/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No....64......2022**
**In the matter of the estate of the late ANNA ELIAS MHEMA of Tambukareli within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by FROLA P. KOMBA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 Day of 5...... 2022
Dated at Dodoma this 22nd day of April 2022

RESIDENT MAGISTRATE I/C

.............................................
**DODOMA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILVANO MANG'ANG'A MAISANGARA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA TUNDRA** yenye usajili namba **T 120 DXN,** CHASSIS NAMBA : **5TFBW5F11JX698874,** ENGINE NAMBA : **3URFE55L.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**DAR/OST/RB/162922/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA CHUO KIKUU (MUHIMBILI UNIVERSITY)



**PATRICK DAMIAN MWAMWONGI**
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha chuo kikuu (muhimbili university) namba ya cheti **DDS000152,** kimeibiwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0628536620**
**MOR/MOR/RB/162570/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MAHAKAMA)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU WILAYA YA ARUMERU**
**SHAURI LA JINAI/MADAI NA 18.YA 2022**
**Mwombaji WILFRED MASIYAYA MDAI/ MLALAMIKAJI**
**Dhidi ya**
**MAREHEMU PAULO MASIYAYA LAIZER MDAIWA/MSHTAKIWA**
**HATI YA KUITWA SHAURINI**
**(MCA Na 2/1984)**

Kwa yeyote anaayehusika na MIRATHI HII TANZANIA BARA NA VISIWANI.
Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka /madai kuwa shahidi kama ifuatavyo

FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA.
UNAAMRIWA NA JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya ALHAMISI tarehe 28/4/2022 saa 03:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa .

USIKOSE KUHUDHURIA
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/f Na. 114 A Sura 15 K/A.Hivyo mahakama inaweza kukuchukulia hatua Kali za kisheria .

HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 25/04/2022

...........
Hati hii imetolewa kwa ombi la WILFRED MASIYAYA.

.....................
HAKIMU
HATI hii imetolewa kwa ombi la Mdai.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**RUFAA NAMBA 72 YA 2021**
**KULWA DIONIZI LUSANA............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SILVANUS P .MWACHA NA**
**SALOME SEBASTIAN MATEMO..........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**SILVANUS P .MWACHA** popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 12/05/2022 mbele ya Mwenyekiti E.MOGOSA wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI Baraza leo tarehe 21/04/2022.

**E.MOGASA**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 49 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late SELINA RAJU MATINYA**

**By 1. MODESTA ALPHONCE MALATI**
**2. .......................................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of MAY ..... 2022
Dated at MOROGORO this 20 day of APRIL ...2022

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
Morogoro


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Jaji anusurika kuuawa Uganda

**Kampala,** UGANDA

JAJI wa Uganda, amenusurika kuuawa katika shambulio la silaha baada ya msafara wake kupigwa risasi mwishoni mwa wiki, mamlaka imesema.

Katika taarifa yake siku ya juzi, mahakama ilisema Jaji Flavian Zeija na timu yake hawakujeruhiwa wakati wa ufyatulianaji wa risasi uliotokea saa 1:00 usiku.

Msemaji wa Mahakama, Jameson Karemani alitaja tukio hilo kuwa la kushtusha na kusema kuwa wahusika watafikishwa mahakamani.

Mamlaka imeanza uchunguzi kuhusu shambulio hilo.

Idadi ya watu wenye hadhi ya juu, Uganda, wamewahi kulengwa na mashambulizi katika miaka ya hivi karibuni. Kesi nyingi bado hazijatatuliwa.

Juni, mwaka jana, waziri mmoja alinusurika jaribio la mauaji lililofanywa na watu wenye silaha waliokuwa kwenye pikipiki katika kitongoji cha Kampala. Binti yake na mlinzi wake waliuawa.

Wengine ambao wameuawa kwa kupigwa risasi katika hali kama hiyo ni pamoja na ofisa mkuu wa polisi, mwendesha mashtaka mkuu na mbunge. **BBC**

## Macron achaguliwa tena Ufaransa

**Paris,** UFARANSA

WAFARANSA kwa mara nyingine, wamepiga kura kwa duru ya pili ya uchaguzi wa urais, juzi, uliowakutanisha rais Emmanuel Macron (pichani) na mwanasiasa wa siasa za mrengo wa kulia, Marine Le Pen.

Hatua ya duru ya pili ni baada ya kushindwa kupatikana mshindi katika duru ya kwanza, wiki mbili zilizopita.



Kulingana na makadirio ya kwanza ya Ipsos, iliyochapishwa juzi, Emmanuel Macron amechaguliwa tena kwa muhula wa pili kwa asilimia 58.2 ya kura.

Kiwango cha ushiriki katika duru ya pili ya uchaguzi wa urais nchini Ufaransa kimefikia asilimia 63.23 juzi, zaidi ya pointi mbili chini ya mwaka wa 2017.

Ushindi huu wa wazi wa Emmanuel Macron, umechangiwa na pengo kubwa sana la mrengo wa kulia kwa asilimia 28 ya kura, kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa kwa duru ya pili tangu mwaka 1969.

Marine Le Pen amepata alama za juu zaidi kwa mrengo wa kulia katika uchaguzi wa urais. **RFI**

# WHO: Chanjo ya kwanza ya Malaria ianze Afrika

**New York,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), linapendekeza upanuzi wa matumizi ya chanjo ya kwanza ya malaria barani Afrika na kwamba inawezekana kuleta mabadiliko katika vita dhidi ya Malaria.

Linatoa pendekezo hilo wakati jana ni siku ya Malaria Duniani. Malaria ni ugonjwa unaozuilika, na unaotibika. Hata hivyo kila mwaka malaria huwakumba zaidi ya watu milioni 200 na kuua zaidi ya 600,000.

Vifo vingi kati ya hivyo karibu nusu milioni, miongoni mwao ni watoto wadogo barani Afrika, ikimaanisha kila sekunde 60 mtoto hufariki kwa malaria.

Licha ya habari hizo, mtazamo wa kudhibiti malaria unatia matumaini kutokana na kutengenezwa kwa chanjo ya kwanza ya malaria duniani.

WHO, linayaita mafanikio hayo ya kihistoria kwa sayansi.

Mpango wa majaribio ulianzishwa mwaka 2019 nchini Ghana, Kenya na Malawi. Tangu wakati huo, WHO linaripoti zaidi ya watoto milioni moja katika nchi hizo tatu wamepokea chanjo ya malaria.

**Kama chanjo hiyo itasambazwa kwa wingi, inakadiriwa kwamba inaweza kuokoa maisha ya watoto wengine hadi 80,000 kila mwaka.**

Mary Hamel, Mkuu wa Mpango wa Utekelezaji wa Chanjo ya Malaria WHO, alisema mpango wa majaribio wa miaka miwili umeonyesha chanjo hiyo ni salama, na kupunguza ugonjwa huo hatari.

"Tuliona kupungua kwa asilimia 30 kwa watoto wanaoletwa hospitali na ugonjwa mbaya wa malaria. Pia tuliona kupungua kwa karibu asilimia 10 kwa vifo vyote vya watoto vinavyosababishwa na malaria.

"Kama chanjo hiyo itasambazwa kwa wingi, inakadiriwa kwamba inaweza kuokoa maisha ya watoto wengine hadi 80,000 kila mwaka".

WHO inaripoti kwamba zitatolewa zaidi ya Dola milioni 155 kusaidia kupanua uzinduzi wa chanjo ya malaria kwa nchi zinazostahiki, GAVI, barani Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Chanjo dhidi ya malaria, ilikuwa ikitengenezwa kabla ya chanjo ya Uviko-19 kutengenezwa.

Hamel alisema WHO imejifunza mengi kutokana na juhudi hizo ambazo zinaweza kutumika katika utengenezaji wa chanjo za malaria siku zijazo.

"Tunajua kumekuwa na mifumo mipya iliyojitokeza tangu chanjo ya Uviko-19, ikijumuisha jukwaa la mRNA na hivi sasa watengenezaji wa mojawapo ya chanjo ya mRNA wanatazamia kutengeneza chanjo ya malaria kwa kutumia jukwaa hilo hilo".

Julai mwaka jana, BioNTech, mtengenezaji wa chanjo ya Pfizer-BioNTech, ilitangaza inataka kuendeleza mafanikio hayo kwa kutengeneza chanjo ya malaria kwa kutumia teknolojia ya mRNA.

Kampuni hiyo ya kutengeneza dawa ilisema inalenga kuanza majaribio ya kimatibabu kufikia mwisho wa mwaka huu. **VOA**



Rais Uhuru Kenyatta akipeana ishara ya salamu na Naibu Rais William Ruto, eneo la bunge, baada ya viongozi kadhaa kukutana kwa ajili ya kuuaga mwili wa aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Mwai Kibaki. **PICHA: NATION MEDIA GROUP**

# Mwili wa Mwai Kibaki wawasili Ikulu

**Nairobi,** KENYA

RAIS Uhuru Kenyatta na mkewe Margaret Kenyatta, wameongoza waombolezaji kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Mwai Kibaki, baada ya kuwasili bungeni, jijini Nairobi.

Mwili wa Kibaki utalala bungeni kwa siku tatu, kuanzia jana Jumatatu hadi Jumatano, ili kuwapa Wakenya muda wa kutoa heshima zao za mwisho.

Mwili wa Rais Kibaki, uliwasili katika majengo ya bunge kwa ajili ya kuagwa.

Naibu Rais William Ruto, mawaziri, mabalozi, wakuu wa jeshi na viongozi wengine wakuu wa serikali, walikuwa ni kati ya viongozi wa kitaifa walioshiriki shughuli hiyo ya mazishi.

Leo na Jumatano, itakuwa zamu ya wananchi wa kawaida kuutazama mwili wa Kibaki ndani ya majengo ya bunge la taifa.

Misa ya kitaifa ya kumuaga Kibaki, itafanywa siku ya Ijumaa Aprili 29, mwaka huu, na atazikwa Jumamosi nyumbani kwake, Othaya Nyeri. **BBC**

# SIMBA QUEENS: KIPIGO YANGA PRINCESS HAKITUTOI RELINI

Na Saada Akida

LICHA ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga Princess, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema kupoteza mchezo huo hakuwezi kuwaondoa katika mipango yao ya kutetea ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo kwenye msimu huu wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Simba Queens juzi ilipoteza mechi yake ya kwanza msimu huu, dhidi ya Yanga Princess ambao wamevunja mwiko kwa kuwafunga Malkia wa Simba hao kwa mara ya kwanza baada ya misimu mitatu ya ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma alisema msimamo wao wa kutwaa ubingwa bado uko pale pale na watahakikisha wanafanya vizuri katika michezo iliyobakia ya ligi hiyo.

Alisema kupoteza mchezo huo kulitokana na kuathiriwa na kadi nyekundu ya mapema aliyopewa beki wao, Julieth Singano, baada ya kumchezea madhambi Clara Luvanga.

"Kipindi cha kwanza tulijaribu, lakini mipango yetu haikufanikiwa, hata hivyo kitendo cha kufungwa dhidi ya Yanga hakijatuondoa katika reli ya mbio zetu za ubingwa, baada ya mechi sita sasa tunaongeza ya saba ya kupambania nafasi ya ubingwa wetu," alisema Nkoma.

Alisema walifanya makosa na Yanga waliyatumia madhaifu yao ya kuwa pungufu na kupata bao la mapema kipindi cha kwanza ambalo lilidumu hadi dakika 90 za mchezo huo zinakamilika.

"Ni mechi yetu ya kwanza kupoteza msimu huu na kufungwa na Yanga ambayo hajawahi kutufunga, lakini pia kufungwa kwa mechi hii, hakujatuondoa katika mbio zetu za ubingwa kwa sababu aliyetufunga tumemzidi pointi 10 na anayeshika nafasi ya pili tukimzidi kwa alama saba," alisema Nkoma.

Naye Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema mechi ilikuwa mzuri kwa pande zote mbili ila anawapongeza wachezaji wake kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu na kumheshimu mpinzani wake.

Alisema ushindi huo kwake umekuwa na maana kubwa mbili, kwanza kuvunja mwiko na uteja mbele ya Simba, lakini pia kuwa timu ya kwanza kuwafunga Simba Queens msimu huu.

"Tulijiandaa kushinda mchezo huu, tumecheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa kumheshimu mpinzani wetu, niwapongeze wachezaji wangu wamefanya kile nilichowaelekeza mazoezini na kuhamishia uwanjani," alisema Edna.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Juma, akimiliki mpira dhidi ya Daniela Ngoyi wa Yanga Princess kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. Yanga ilishinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Ligi ya Wanawake Zanzibar walia ukata

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, wamesema licha kuanza mzunguko wa pili wa ligi hiyo, wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ukata.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Kamati ya Soka la Wanawake Zanzibar, mzunguko wa pili wa ligi hiyo utaendelea mapema Mei 10, mwaka huu na itachezwa katika viwanja vya Unguja na Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa viongozi wa timu hizo, Suleiman Mohmed Boko, ambaye ni Katibu wa Dunga Queens, alisema mzunguko huu timu zinatakiwa kwenda kucheza Uwanja wa Gombani katika mechi zake za ugenini.

Alisema katika mzunguko huu timu zinahitaji fedha kwa ajili ya kusafiri kutoka Kisiwani Unguja kuelekea Pemba pamoja na fedha nyingine za kujikimu kwa kipindi ambacho timu hiyo itakuwa kisiwani humo.

Boko alisema mpaka sasa timu hiyo haijaweza kukamilisha bajeti yake waliyoiandaa katika mzunguko huu wa pili hasa kwa mechi mbili watakazoenda kucheza Pemba.

"Tunajiandaa na mzunguko wa pili ambao utakuwa na gharama zaidi kwa ajili ya kusafiri, lakini pia zitahitajika fedha za kujikimu kwa wachezaji pindi wakiwa Pemba, hivyo tunaendelea na jitihada kuona tunapata walau wafadhili kwa ajili ya kufanikisha mzunguko wa pili,"alisema.

Hata hivyo, amewaomba wadau wa soka hapa Zanzibar kujitokeza kuzisaidia timu za wanawake pamoja na kuzipa hamasa ili zisonge mbele pamoja na kupata timu nyingi za wanawake ikilinganishwa na sasa ambapo kwa Zanzibar nzima kuna timu 10 tu.

# Scolastica atwaa tena ubingwa baiskeli

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BINGWA mara tatu mfululizo wa michuano ya Kombe la Mei Mosi, Scolastica Hamis wa timu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), ametwaa tena ubingwa wa kuendesha baiskeli kwa upande wa wanawake baada ya juzi kumaliza kinara kwenye mbio za kilometa 15 zilizoanzia eneo la Chisichiiri na kumalizikia Isanga Plaza.

Scolastica, ambaye ni bingwa wa mbio hizo kwa miaka mitatu mfululizo, amesema amekuwa akitwaa ubingwa huo mara kwa mara katika michuano hii na ile ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), kutokana na kuupenda mchezo huo na pia kufanya mazoezi kwa bidii akizingatia maelekezo ya makocha wake.

"Huu mchezo naupenda sana nahisi nisipocheza ninaumwa ndio maana nimekuwa nikishiriki sana katika mashindano mbalimbali na ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, sekta yangu ya Uchukuzi na taasisi yangu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa kunipa ushirikiano na msaada mkubwa wa kushiriki kwenye michuano hii na mingine," alisema Scolastica.

Ushindi wa pili kwa wanawake umechukuliwa na Bertha Mtanga wa TEMESA na ushindi wa tatu umekwenda kwa Alavuya Mtalima wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa upande wa wanaume, mchezaji Steven Sanga wa timu ya Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, ametwaa ubingwa baada ya kuwabwaga wachezaji wakongwe na wazoefu katika mbio za kilomita 21 zilizoanzia eneo la Matumburu na kumalizikia Isanga Plaza.

Sanga alisema siri ya ushindi wake ni kumtanguliza Mungu mbele, pamoja na kufanya mazoezi kwa bidii kwa kufuata maelekezo ya makocha.

"Ninamshukuru sana Mungu kwa kutwaa ushindi wa kwanza maana mbio zetu zilikuwa na ushindani mkubwa sana, hivyo ninaahidi kuendelea kutwaa ubingwa katika michuano mingine ijayo," alisema Sanga.

Wazoefu walioangukia pua na kushika nafasi ya pili ni Hassan Ligoneko wa Wizara ya Afya na aliyeshika nafasi ya tatu ni Chaptelel Muhumba wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi).

Mbio hizo zimeshirikisha wachezaji 18 kwa upande wa wanaume na 10 kwa upande wa wanawake.

Michuano hii ambayo inatarajia kufikia kilele Ijumaa wiki hii, iliendelea jana katika Uwanja wa Jamhuri kwa michezo ya jadi ya kucheza draft, bao na karata.

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO KUTIMULIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inatarajia kumtimua kocha wake, Mauricio Pochettino huku kocha wa Tottenham Antonio Conte akitajwa kumrithi. ***(Le Parisien via GFFN)***

### OSIMHEN HUYOOO ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumnasa mshambuliaji wa Napoli na Nigeria ,Victor Osimhen, 23. ***(Gazzetta dello Sport via HITC)***

### KOUNDE KUTUA CHELSEA

CHELSEA huenda ikafufua tena mbio zake za kumnasa mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23 katika dirisha lijalo baada ya kuthibitishwa kuwa Antonio Rudiger kuondoka klabuni hapo. ***(Football London)***

### JESUS AMEGOMA

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25, amegoma kubakia City baada ya msimu kumalizika. ***(Guardian)***

### HUBERS AWINDWA LEEDS

LEEDS United imewatuma wasaka vipaji wake kumuangalia mlinzi wa kati wa Cologne ya Ujerumani, Timo Hubers mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### SATRIANO AGOMBEWA

CHELSEA na Tottenham zinamfuatilia mshambuliaji wa Inter Milan, Martin Satriano mwenye umri wa miaka 21. Mruguay huyu kwa sasa anakipiga kwa mkopo katika Klabu ya Ufaransa ya Brest. ***(Mirror)***

### PAQUETA KUAMUA LYON

KIUNGO wa kimataifa wa Brazil anayehusishwa na Newcastle United, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 24, ameiambia klabu yake ya sasa ya Lyon kwamba atafanya uamuzi wa hatma yake mwishoni mwa msimu. ***(Evening Chronicle)***

### KEAN KUWA KOCHA

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Roy Keane anatajwa kuwania nafasi ya kukinoa kikosi cha Hibernian. ***(Times)***

### DYBALA ATAKIWA ROMA

AS Roma imeingia katika mbio za kumsaka mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paolo Dybala mwenye umri wa miaka 28. ***(Fichajes)***

### ISCO KUTUA BETIS

REAL Betis wanajaribu kumsajili kiungo mchezaji wa Real Madrid na Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 30. ***(Marca)***

### ELNENY KUBAKI ARSENAL

KIUNGO wa Misri, Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 29, amesema anaweza kusaini mkataba mpya wa kubakia Arsenal hata kama hatapewa uhakika wa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza. ***(Irish Examiner)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# BARCA WAKUTANA RASMI NA WAKALA WA RUDIGER

## Tulikuwa na mkutano naye, lakini pia anawakilisha wachezaji wengine, hivyo...

**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa Barcelona, Mateu Alemany, amethibitisha kufanya mazungumzo na wakala wa Antonio Rudiger, lakini amesisitiza mustakabali wa beki huyo wa Chelsea haukujadiliwa wakati wa mkutano huo.

**Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel alifichua baada ya ushindi wa dakika za lala salama dhidi ya West Ham Jumapili kuwa Rudiger ana nia ya kuondoka katika klabu hiyo mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.**

Tuchel alipendekeza kuwa uamuzi wa Rudiger ulichangiwa na vikwazo vya kifedha vilivyowekwa kwa Chelsea huku mmiliki mpya wa kumrithi Roman Abramovich akitafutwa.

Barcelona ni miongoni mwa timu ambazo zimehusishwa na nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani, pamoja na wapinzani wao, Real Madrid, Juventus na Paris Saint-Germain.

Akizungumza kabla ya pambano la nyumbani la Barca kwenye LaLiga dhidi ya Rayo Vallecano baadaye Jumapili, Alemany alisema wamekutana na wakala wa beki huyo wa kati.

"Tulikuwa na mkutano na wakala wake, lakini pia anawakilisha wachezaji wengine," alisema Alemany akiiambia Movistar.

"Hatukuzungumza kuhusu hali yake, lakini kuhusu mambo mengine mengi kwa sababu wakala wake anawakilisha wachezaji wengi. Ni sheria ya nyumbani kutozungumza kuhusu wachezaji wa klabu nyingine."

Barca wamelazimika kukabiliana na ukomo wa kifedha wao wenyewe, lakini bado waliweza kuwasajili Ferran Torres, Pierre-Emerick Aubameyang, Dani Alves na Adama Traore, Januari. Na wababe hao wa Katalunya, ambao watamaliza msimu huu wa 2021-22 bila taji, wanatarajiwa kuwa na shughuli nyingi katika dirisha lijalo la uhamisho.

"Tayari tuna mawazo ya hali ya juu," Alemany alisema. "Tutafanya tathmini ya pamoja ligi inapomalizika au wakati msimamo wetu umewekwa.

"Majira ya joto yaliyopita yalikuwa magumu kwani tulizuiliwa katika kiwango cha 'fair play'. Sasa tumeridhishwa na timu ya makocha na tunakusudia kufanya kiwango kikubwa cha ubora.

"Nia yetu ni kutengeneza timu ya ushindani kwa mwaka ujao."


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,198

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
REAL MADRID
1 | 1.51
X | 4.19
2 | 5.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP ASIFU KIWANGO CHA ORIGI



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alifurahishwa na juhudi za Divock Origi wakati wa ushindi wa mabao 2-0 wa timu yake dhidi ya Everton, Jumapili.

Origi amefunga mabao sita dhidi ya Everton katika michuano yote akiwa na Liverpool, ambayo ni mara mbili ya mabao aliyofunga dhidi ya timu nyingine yoyote.

Akizungumza na Sky Sports baada ya ushindi huo, Klopp alimmwagia sifa Origin na kusema ni mchezaji wa kimataifa.

"(Origi) ni mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa," alisema.

"Yeye ndiye mkamilishaji wetu bora, bila shaka - alikuwa siku zote, na kila mtu angesema hivyo.

"Unamuona anafanya mambo ya aina hii kwenye mazoezi, halafu hayupo kwenye kikosi kwa sababu ya ubora wa wachezaji wengine, ni ngumu sana.

"Hatutawahi kukosa mchezaji kama yeye kwa sababu akiondoka, atang'ara popote atakapoenda ... yeye ni gwiji na atabaki kuwa gwiji milele."



## Pioli ataka wachezaji wasifiwe

**MILAN,** Italia

STEFANO Pioli anaamini kuwa wachezaji wake wa AC Milan hawapati sifa wanazostahili baada ya bao la dakika za lala salama la Sandro Tonali kuhitimisha ushindi muhimu wa 2-1 dhidi ya Lazio, Jumapili.

Olivier Giroud alikuwa amesawazisha bao la mapema la Ciro Immobile kwenye Uwanja wa Olimpico, lakini ilionekana kama Rossoneri hao wesingeibuka na ushindi baada ya kukosa nafasi nyingi za wazi.

Lakini Tonali aliibuka kuwa shujaa katika dakika ya pili ya muda wa nyongeza na kupata ushindi ambao uliwanyanyua Milan pointi mbili juu ya Inter kileleni mwa msimamo, ingawa wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Matokeo hayo yalimaanisha kuwa wameshinda michezo mitatu dhidi ya vijana wa Maurizio Sarri katika msimu mmoja (miwili katika Serie A, mmoja Coppa Italia) kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2004-05.

Akizungumza na DAZN baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Pioli alizungumzia kujivunia kwake kutokana na jitihada za wachezaji wake na kusisitiza kuwa hawapokei pongezi wanazostahili.

"Ninajivunia sana wachezaji wangu na kama ningekuwa katika viatu vyao, ningekasirika," alisema.

"Watu hawawapi hongera za kutosha. Kwa miaka mingi, wamekuwa wakijidhihirisha katika kiwango cha juu.

3,475,840

# JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/04/22 | 17:00 | Watford vs Burnley | 2.51 | 3.20 | 2.71 |
| 02. 30/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Brighton | 2.64 | 3.04 | 2.69 |
| 03. 30/04/22 | 17:00 | Southampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 30/04/22 | 17:00 | Barnsley vs Preston | 2.77 | 3.27 | 2.42 |
| 05. 30/04/22 | 17:00 | Coventry vs Huddersfield | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 06. 30/04/22 | 19:00 | Sampdoria vs Genoa | 2.46 | 3.18 | 2.79 |
| 07. 30/04/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 08. 01/05/22 | 15:00 | Elche vs Osasuna | 2.99 | 3.09 | 2.42 |
| 09. 01/05/22 | 15:30 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.59 | 3.43 | 2.49 |
| 10. 01/05/22 | 16:00 | Empoli vs Torino | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 01/05/22 | 17:15 | Granada vs Celta Vigo | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 12. 01/05/22 | 19:30 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 2.96 | 3.06 | 2.47 |
| 13. 01/05/22 | 21:00 | Waalwick vs Groningen | 2.68 | 3.33 | 2.46 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 26/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4912 | Arba Minch Kenema vs Fasil Kenema | 4.66 | 2.96 | 1.83 |
| 15:00 | 5142 | Watford U23 vs QPR U23 | 2.34 | 4.19 | 2.31 |
| 17:00 | 3540 | Tobol Kostanay vs Astana | 2.48 | 2.97 | 2.77 |
| 18:00 | 3200 | Dziugas vs Banga Gargzdai | 1.61 | 3.69 | 4.76 |
| 18:00 | 3767 | Varnsdorf vs SK Lisen | 2.33 | 3.22 | 2.78 |
| 18:00 | 4158 | AEK Larnaca vs Ethnikos Achnas | 1.30 | 4.57 | 8.76 |
| 19:00 | 1014 | Universitatea Cluj vs Petrolul Ploiesti | 2.26 | 2.78 | 3.36 |
| 19:00 | 1318 | Vindbjart vs Start 2 | 1.70 | 4.67 | 3.35 |
| 19:00 | 2291 | AS Trencin vs Zlate Moravce | 1.58 | 3.99 | 4.67 |
| 19:00 | 2861 | Chrobry Glogow vs Resovia Rzeszow | 2.67 | 2.96 | 2.58 |
| 19:00 | 3063 | Anorthosis Famagusta vs Omonia Nicosia | 2.04 | 3.02 | 3.60 |
| 19:00 | 4221 | Zaglebie Sosnowiec vs Miedz Legnica | 3.35 | 3.25 | 2.03 |
| 19:30 | 3241 | TSV Hartberg vs SCR Altach | 2.04 | 3.26 | 3.31 |
| 19:30 | 3718 | WSG Wattens vs LASK Linz | 4.29 | 3.75 | 1.67 |
| 19:30 | 5260 | TSV Rain/Lech vs Schweinfurt | 4.66 | 4.08 | 1.56 |
| 19:30 | 5886 | Josko Ried vs Admira Wacker | 2.55 | 3.20 | 2.70 |
| 20:00 | 1736 | Grorud IL 2 vs Stabaek Fotball 2 | 2.28 | 3.99 | 2.43 |
| 20:00 | 2596 | Nomme Kalju vs Tallinna JK Legion | 1.11 | 7.38 | 16.50 |
| 20:00 | 2843 | Kalmar vs Norrkoping | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 20:00 | 4549 | Orebro SK vs Halmstads BK | 2.67 | 3.22 | 2.67 |
| 20:00 | 4832 | Lorenskog vs Mjondalen 2 | 1.65 | 3.89 | 4.19 |
| 20:00 | 5148 | Skeid Fotball 2 vs Lyn Oslo | 4.77 | 4.87 | 1.46 |
| 21:00 | 1134 | Qalali vs Bahrain Club | 3.75 | 3.41 | 1.85 |
| 21:00 | 2081 | Defensores de Belgrano vs Satsaid | 2.02 | 3.89 | 2.87 |
| 21:00 | 2599 | Sheffield United U23 vs Millwall U23 | 1.35 | 4.87 | 6.43 |
| 21:30 | 1489 | Widzew Lodz vs Korona Kielce | 2.05 | 3.22 | 3.32 |
| 21:35 | 1868 | Justo Jose De Urquiza vs Ituzaingo | 2.52 | 2.52 | 3.25 |
| 21:45 | 1562 | Southend vs Boreham Wood | 2.76 | 3.01 | 2.56 |
| 21:45 | 1739 | Sutton United vs Crawley Town | 1.87 | 3.47 | 3.87 |
| 21:45 | 1839 | Sunderland vs Rotherham | 2.28 | 3.27 | 2.98 |
| 21:45 | 2132 | Dover vs Notts County | 9.89 | 5.34 | 1.26 |
| 21:45 | 2711 | Swindon Town vs Forest Green | 2.36 | 3.37 | 2.78 |
| 21:45 | 3071 | Fleetwood Town vs Sheffield Wed | 5.35 | 3.71 | 1.60 |
| 21:45 | 3085 | Al Shabbab-Al vs Tadamun Buri | 1.02 | 10.72 | 34.11 |
| 21:45 | 3406 | Weymouth vs Wrexham | 8.28 | 4.83 | 1.32 |
| 21:45 | 3605 | Mansfield vs Stevenage | 1.64 | 3.71 | 4.95 |
| 21:45 | 3900 | College 1975 FC vs Europa Point FC | 1.91 | 3.79 | 3.21 |
| 21:45 | 3949 | Barnsley vs Blackpool | 2.78 | 3.27 | 2.41 |
| 21:45 | 4071 | Chester vs York City | 2.72 | 3.31 | 2.32 |
| 21:45 | 4251 | Exeter vs Barrow | 1.59 | 3.72 | 5.55 |
| 21:45 | 4458 | Fulham vs Nottingham | 1.71 | 3.63 | 4.57 |
| 21:45 | 4637 | Concord Rangers vs Slough Town | 2.06 | 3.54 | 3.01 |
| 21:45 | 4668 | Swansea vs Bournemouth | 3.67 | 3.37 | 1.96 |
| 21:45 | 4880 | Portsmouth vs Wigan | 2.88 | 3.18 | 2.39 |
| 21:45 | 5492 | Alfreton vs Curzon | 1.84 | 3.55 | 3.65 |
| 21:45 | 5691 | Bromley vs Aldershot | 2.00 | 3.40 | 3.45 |
| 22:00 | 2372 | Manchester City vs Real Madrid | 1.51 | 4.19 | 5.59 |
| 22:30 | 4273 | Ismaily SC vs Enppi Club | 2.30 | 2.84 | 3.48 |
| 22:30 | 4811 | National Bank vs Eastern Company SC | 1.89 | 3.10 | 4.50 |
| 22:30 | 5049 | Arab Contractors vs El Ittihad Alexandria | 2.89 | 2.84 | 2.65 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM FC YAPIGIA HESABU POINTI SITA KANDA YA ZIWA

Na Saada Akida

BAADA ya kujiondoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, hesabu zake amezielekeza kuwania nafasi ya tatu, lakini kwa sasa akiweka wazi anahitaji pointi sita za mechi mbili za ugenini kwanza.

Azam FC imeshuka dimbani Ijumaa wiki hii kuivaa Geita Gold FC ambayo itakuwa katika uwanja wake wa nyumbani wa Namkumbu uliopo mjini Geita, na baada ya hapo 'Wanalambalamba' hao watafunga safari kuelekea Bukoba kuvaana na Kagera Sugar Mei 3, mwaka huu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, kocha huyo alisema maandalizi ya mechi hizo yanaendelea vizuri na wanajipanga kuhakikisha wanapata pointi sita za michezo hiyo miwili ya ugenini.**

Alisema mechi zimekuwa na ushindani mkubwa na wanapambana kuhakikisha timu inapata matokeo mazuri katika michezo hiyo ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kumaliza ligi katika nafasi tatu za juu.

"Tunatakiwa kushinda mechi zilizopo mbele yetu ili kufikia malengo hayo, tunaenda kucheza mechi mbili za ugenini, ni muhimu kutafuta matokeo ili kujiweka katika nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa ligi," alisema Moallin.

Alisema wamepata mechi ya kirafiki ambayo imempa mwanga wa kuona mapungufu ya kikosi chake kuelekea mchezo dhidi ya Geita Gold FC.

Azam FC kwa sasa ipo nafasi ya nne ikiwa na alama 28, moja nyuma ya Namongo FC iliyopo nafasi ya tatu, lakini ikiwa imeshuka dimbani mechi mbili zaidi ya Wanalambalamba hao.



Wachezaji wa Azam FC, wakiwa mazoezini kujiandaa na mechi za Ligi Kuu. **MPIGAPICHA WETU**

# Jeshi Stars, Tanesco zafanya kweli Wavu

Na Saada Akida

TIMU ya Jeshi Stars na Tanesco zimeibuka na ushindi katika michezo yao ya Ligi ya Mpira wa Wavu Mkoa Dar es Salaam iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa, Dar es Salaam.

Timu ya Wanawake ya Jeshi stars iliibuka na ushindi wa seti 3-0 dhidi ya UDSM, huku upande wa wanaume Tanesco ikishinda seti 3-1 dhidi ya UDSM.

Matokeo mengine ya mechi za wanawake, Wazo ilikubali kichapo cha seti 3-0 dhidi ya Star Girls, wakati kwa wanaume, Maafande wa Jeshi Stars wakiwapigisha kwata maafande wenzao, Nyika kwa seti 3-0.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea leo kwa michezo miwili kupigwa kwenye uwanja huo, mchezo wa kwanza kwa wanawake utakuwa kati Star Girls dhidi ya Magereza, wakati upande wa wanaume Chui wakimenyana na Jeshi stars

# Michezo

Jumanne Aprili 26, 2022

Nipashe




Barca wakutana na wakala wa Rudiger UKURASA 21

JUU KWA JUU...



Kiungo wa Simba, Sadio Kanoute, akiwania mpira kwa kichwa na mchezaji wa Orlando Pirates, kwenye mechi ya robo fainali Mkondo wa pili wa Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini juzi. Orlando ilishinda kwa mikwaju ya penalti 4-3 baada ya dakika 90 kumalizika wakishinda 1-0 kama ambavyo Simba ilishinda nyumbani, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Klopp akunwa na kiwango cha Origi

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alifurahishwa na juhudi za Divock Origi wakati wa ushindi wa mabao...



HABARI UK 22

## Azam FC yataka 6 Kanda ya Ziwa

**Na Saada Akida**

BAADA ya kujiondoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid...



HABARI UK 23

# Pablo awapoza mashabiki Simba

## ●●● Asema subirini tutarudi kwa kishindo michuano CAF, atoa sababu kipigo Sauzi...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema wamekubali kushindwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa kutolewa na timu ngumu ya Orlando Pirates, lakini akitamba kuwa atarejea msimu ujao na timu yake wakiwa imara zaidi.

**Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini, Pablo ameipongeza Orlando kwa kutinga hatua ya nusu fainali, lakini pia akiwapongeza wachezaji wa timu yake ya Simba kwa kupambana kwa dakika zote 180 nyumbani na ugenini dhidi ya timu ambayo iliwazidi kwa kila kitu.**

"Kwanza kabisa napenda kupongeza Orlando Pirates, siyo kama alivyofanya kocha mwenzangu wiki moja iliyopita kwa kuzungumzia vikwazo, kuelezea mapokezi na VAR, walikuwa wazuri zaidi yetu kwa dakika 180, walicheza soka zuri kushinda sisi na walituzidi. Kwa mara ya kwanza nimeona wachezaji wa Simba wakishindana na kupambana kwenye mchezo mgumu, tena ugenini kwenye mashindano haya na kama tulivyokuwa 11 kwa 11 kule Dar es Salaam, licha ya kuwa vinara wa magoli kwenye hatua za makundi, hivyo ikabidi tujiimarishe zaidi," alisema Pablo.

Alisema kuwa tatizo lilikuja walipopoteza mchezaji mmoja, Chris Mugalu ambaye alizawadiwa kadi nyekundu kwa kumkanyaga beki wa Orlando Pirates.

"Nawapongeza sana wachezaji wangu kwa moyo wa kujitolea kwa ajili ya timu licha ya kucheza pungufu uwanjani kwa muda mrefu, ulikuwa mchezo mgumu wakuvutia, lakini tutasubiri kwa mwaka mmoja kufikia malengo yetu.

"Kuanzia hapo tulijitahidi kuzuia, tukaenda kwenye penalti ambazo hazina mwenyewe, ni suala la kiwango, umakini na bahati. Najivunia kufanya vizuri kwa wachezaji wangu na najipanga kwenye michuano mingine, kama siyo hii basi ni Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Simba ilitolewa juzi kwenye hatua ya robo fainali kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya timu hizo kufungana bao 1-1, kila timu ikishinda bao 1-0 nyumbani.

Baada ya kutolewa, Simba iliwasili jana nchini kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba inaweza kuiwakilisha tena nchi kwenye michuano ya kimataifa; Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao endapo itamaliza nafasi ya kwanza ama ya pili kwenye Ligi Kuu Bara kwani msimu ujao Tanzania itaingiza tena timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF.

Hiyo ni kutokana na juhudi zilizofanya Simba katika michuano hiyo na kufanikiwa kuiongezea Tanzania pointi, hivyo kuwa miongoni mwa nchi 12 ambazo kila moja itaingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya Afrika; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >